

**MATUMIZI YA LUGHA KATIKA SIASA: UMUHIMU WA MIELEKEO KATIKA
KUCHAGUA LUGHA YA MJADALA BUNGENI KWENYE KAUNTI YA SIAYA**

ODUOR ATIENO WINNIE

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SHAHADA ZA JUU ILI
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA
UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA

JUNI, 2025

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote kwenye Chuo Kikuu kingine kile.

Saini.....

Tarehe 01/07/2025

Oduor Atieno Winnie

MAKI/2021/83692

IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa madhumuni ya kutahiniwa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili kwa idhini yangu kama msimamizi.

Dkt. Alex Umbima Kevogo.

Chuo Kikuu cha Garissa.



Sahihi

Tarehe: 31/6/2025

TABARUKU

Kwa wazazi wangu wapendwa Bwana Charles Oduor Omondi na Bi. Roseline Akinyi Otuoma Mwanahamisi. Kwa mwanangu Winston Prince pamoja na ndugu zangu akiwemo Frankline Ouma Oduor.



SHUKRANI

Ningependa kuanza kwa kumshukuru Maulana kwa neema yake na kunijalia afya njema katika harakati nzima ya kuitayarisha kazi hii.

Namshukuru msimamizi wangu Daktari Alex Umbima Kevogo kwa kunielekeza na kunipa mwongozo faafu bila kusita. Pia, kwa uvumilivu wake kila nilipozembea kazini kwani hakusita kunitia moyo na kunihimiza kujitahidi kuiendeleza kazi hii na hata kuweza kunisaidia kutatua changamoto mbalimbali niliyoyapitia. Usaidizi wake hauwezi kukisiwa wala kulipwa. Langu kwake ni kumwomba Jalali ambariki na aendelee kumhifadhi na kumjalia hali njema ili aendelee kuwaongoza na kuwaelekeza wakufunzi wengine wengi.

Shukrani zaidi ziende kwa Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa kunipa nafasi ya kuendeleza masomo yangu na pia kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili wakiwemo Bi Gladys Wanjiru, Daktari Stanley Adika Kevogo, Daktari Jackline Murimi, Daktari Miriam Nderitu na wengineo. Shukrani zangu za kipekee ziwaendee wazazi wangu Bwana Charles na Bi. Roseline pamoja na mwanangu Winston walioniombea kila uchao na kunitakia mema kwa kunitia moyo kila nilipojihisi mnyonge na kutaka kukata tamaa. Rabuka awabariki na awalinde daima dawamu. Shukrani nyingine ziwaendee Bwana Kennedy na Jeff bila kumsahau kaka Rodgers kwa huduma ya mtandao na mielekeo ya hapa na pale nilipokuwa natayarisha kazi yangu na hata wakati wa kuiwasilisha kikaoni. Nawashukuru kwa kunisaidia kuichapisha kazi hii. Mungu awabariki na awe nanyi.

Nikihitimisha, ningependa kuwashukuru wakufunzi wenzangu ambao ni pamoja na: Josephine Kisangau , Muli Solomon, Jude Muli, Edith Mwangi, Wesley Ngige, Nancy Kim, Nancy Lazline na Faith kwa kuwepo kila wakati nilipohitaji mwelekeo wowote kutoka kwenu kama vile kudurusu pamoja na kuhimizana. Nawatakieni kila la heri mnapoendelea na safari hii ya kubukua. Kwa wale ambao sijawataja hapa, naomba mniwie radhi. Ni kweli kuwa walionisaidia kwa namna moja au nyingine kuikamilisha kazi hii ni wengi na huenda nikakosa kuwataja wengine. Ninawashukuru kwa dhati.

IKISIRI

Mielekeo katika uteuzi wa lugha ya mijadala ya wajumbe bungeni imekuwa ikiathiriwa na hali iliyopo kwa wakati fulani kwani ni lazima kila mjumbe atetee hoja yake kwa dhati ili kukidhi matakwa ya waliowachagua. Utafiti huu ulinuia kuchanganua baadhi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha ya mijadala ya wajumbe bungeni katika kaunti ya Siaya. Ili kubaini ukweli wa utafiti huu, malengo manne mahususi yaliangaziwa. Malengo hayo ni pamoja na: kuchunguza ikiwa mielekeo inachangia hali ya kuteua lugha inayotumika wakati wa mijadala ya wajumbe bungeni katika kaunti ya Siaya, kuchunguza ikiwa kuna lugha fulani ambayo wajumbe hupendelea wanapokuwa kwenye mijadala yao bungeni katika kaunti ya Siaya, kuangazia iwapo wajumbe wa serikali ya kaunti ya Siaya wana sababu maalumu zinazowapelekea kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine katika mijadala yao bungeni na kuchunguza iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia wajumbe wa kaunti ya Siaya kutumia lugha ya Kiswahili kufanikisha mawasiliano katika muktadha wa mijadala bungeni. Utafiti huu uliongozwa na nadharia za Vitendo Vilivyofikiriwa iliyoasisiwa na Fishben na Azjen na ile ya Utambulisho iliyoasisiwa na Giles. Mihimili pamoja na sifa za nadharia hizi zilitusaidia kufikia malengo ya utafiti. Mtafiti alishughulika na utafiti wa maktabani na wa mtandaoni ambapo data ilipatikana kutokana na tasnifu zilizoandikwa kuhusu jamii za ukanda wa ziwani ulio magharibi mwa Kenya. Vilevile, utafiti wa nyanjani ulitumika pamoja na mbinu anuwai za kimaelezo katika kuchambua data na kuiwasilisha kwa lugha ya nathari kuambatana na malengo ya utafiti. Maarifa yaliyopatikana katika utafiti huu yatakuwa na mchango mkubwa katika maarifa yaliyopo kuhusu masuala ya mielekeo katika uteuzi wa lugha katika jamii. Pia, matokeo ya utafiti huu yatafaidi viongozi wa kisiasa katika jimbo hili la Siaya na taifa zima la Kenya katika mchakato wa kujenga uwiano wa makabila yaliyo na lugha na tamaduni mbalimbali.

ABSTRACT

The choice of language during the debates has been affecting the debaters in the parliament since they must choose the language wisely to defend their points to fulfil the needs and demands of the voters who send them in their specific parliament as their representatives. This research is aimed to unearth the truth of some of the basis towards the choice of language of debate by the members of county assembly of Siaya county of Kenya. To come up with the truth of this matter, four major objectives were put forward. These objectives included; to investigate whether attitudes of the debaters lead to the choice of the language to be used in debate in the county assembly of Siaya, to investigate whether there is a specific language preferred by the debaters in their debates in parliament in the county assembly of Siaya, to analyze whether the debaters of the county assembly of Siaya have a specific reason that leads them to prefer one language to the other in their debates in parliament by the debaters and analyze whether there are possible challenges that the debaters may come across in the use of Kiswahili language during the parliament proceedings in the said county. The theories of Reasoned Action of Fishbein and Azjen and that of Communication Accommodation of Giles guided the researcher to accomplish her objectives. The foundations of this theory gave the light to the researcher as she visited both the library and the field to gather information to come up with the truth of her targetted objectives. During the whole research process, purposeful sampling was employed together with deceptive methods of analyzing and presenting the data in the prose and clear language were utilized as per the set objectives. The knowledge acquired after the research will supplement the already existing knowledge on the basis of language of choice in the community. At the same time, the results of the study will be of great help to the political leaders of Siaya county and in Kenya as they endeavor to unite Kenyans of different tribes and traditions.

YALIYOMO

| | |
|---|------------|
| TABARUKU | iii |
| SHUKRANI..... | iv |
| IKISIRI..... | v |
| ABSTRACT | vi |
| YALIYOMO | vii |
| ORODHA YA VIELELEZO..... | i |
| ORODHA YA MAJEDWALI..... | ii |
| VIFUPISHO NA AKRONIMU ZILIZOTUMIKA..... | iii |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| MSINGI WA UTAFITI..... | 1 |
| 1.0 Utangulizi | 1 |
| 1.1 Usuli wa Mada..... | 1 |
| 1.2 Suala la Utafiti..... | 5 |
| 1.3 Malengo ya Utafiti | 6 |
| 1.4 Maswali ya Utafiti..... | 7 |
| 1.5 Sababu za Kuteua Mada..... | 7 |
| 1.6 Umuhimu wa Utafiti..... | 9 |
| 1.7 Mawanda na Mipaka ya Utafiti..... | 10 |
| 1.8 Maelezo ya Istilahi Maalumu zilizotumika..... | 10 |
| SURA YA PILI | 12 |
| MWAUO WA MAANDISHI..... | 12 |
| 2.0 Utangulizi | 12 |
| 2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada..... | 12 |
| 2.2 Misingi ya Nadharia..... | 17 |
| 2.3 Hitimisho..... | 21 |
| SURA YA TATU | 22 |
| MBINU ZA UTAFITI..... | 22 |
| 3.0 Utangulizi | 22 |
| 3.1 Muundo wa Utafiti | 22 |
| 3.2 Eneo la Utafiti | 22 |

| | |
|--|-----------|
| 3.3 Walengwa wa Utafiti..... | 23 |
| 3.4 Sampuli na Uteuzi wa Sampuli | 24 |
| 3.5 Mbinu na Vifaa vya Kukusanya Data | 25 |
| 3.5.1 Utafiti wa Maktaba..... | 25 |
| 3.5.2 Utafiti wa Nyanjani | 26 |
| 3.6 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Matokeo ya Data itakayokusanywa..... | 26 |
| 3.7 Maadili ya Utafiti | 27 |
| 3.8 Hitimisho..... | 28 |
| SURA YA NNE | 29 |
| UCHANGANUZI WA DATA, UFAHIRI NA MATOKEO YA UTAFITI..... | 29 |
| 4.0 Utangulizi | 29 |
| 4.1 Mukstadha wa Kiisimu wa Eneo la Utafiti | 29 |
| 4.1 Uchanganuzi wa Data Kuhusu Mielekeo ya Lugha ya Wajumbe..... | 29 |
| 4.1.1 Urahisi wa Kujifunza Kiswahili | 32 |
| 4.1.2 Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya kutoa Hoja katika Mijadala Bungeni | 33 |
| 4.1.3 Uelewekaji wa Ujumbe unaowasilishwa katika Lugha ya Kiswahili | 35 |
| 4.1.4 Dhima ya Kiswahili katika Maendeleo ya Taifa la Kenya..... | 36 |
| 4.1.5 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari..... | 37 |
| 4.1.6 Matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika Mijadala Bungeni | 38 |
| 4.1.7 Ugumu wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha katika Mijadala Bungeni | 40 |
| 4.1.8 Athari za Makosa ya Kimatamshi katika Matumizi ya Kiswahili | 41 |
| 4.1.9 Kuchanganya Lugha wakati wa Kutoa Hoja Bungeni | 43 |
| 4.1.10 Utoaji Hotuba kwa Wananchi kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili | 44 |
| 4.1.11 Uamuzi wa Kuchangua Kutumia Kiingereza au Kiswahili | 45 |
| 4.1.12 Ujasiri wa Kutumia Lugha ya Kiswahili Bungeni | 47 |
| 4.1.13 Matumizi ya Kiingereza katika Vyombo vya Habari..... | 48 |
| 4.1.14 Hisia za Unyonge wakati wa kuzungumza Kiswahili | 49 |
| 4.1.15 Ujuzi na Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili Fasaha..... | 51 |
| 4.1.16 Ufasaha wa Lugha ya Kiswahili..... | 53 |
| 4.1.17 Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari..... | 54 |
| 4.1.18 Matumizi ya Kiswahili katika Ofisi na Mazingira ya Kazini..... | 55 |
| 4.1.19 Matumizi ya Kiswahili Kitaifa..... | 57 |

| | |
|---|-----------|
| 4.1.20 Kiswahili ni Chombo cha Umoja wa Wakenya | 58 |
| 4.2 Uchanganuzi wa Sababu za Mielekeo ya Wajumbe | 59 |
| 4.2.1 Urahisi wa Kujifunza Kiswahili | 60 |
| 4.2.2 Matumizi ya Kiswahili Kutoa Hoja katika Mijadala Bungeni | 60 |
| 4.2.3 Lugha ya Kiswahili na Uelewaji Ujumbe unaowasilishwa kwa Urahisi | 61 |
| 4.2.4 Dhima ya Kiswahili katika Maendeleo ya Taifa la Kenya..... | 62 |
| 4.2.5 Vipindi Vinavyotolewa katika Lugha ya Kiswahili kwenye Vyombo vya Habari..... | 63 |
| 4.2.6 Matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika Mijadala Bungeni | 64 |
| 4.2.7 Ugumu wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha..... | 65 |
| 4.2.8 Matamshi ya Kiswahili na yanavyoathiri Matumizi yake..... | 65 |
| 4.2.9 Hali ya Kuchanganya Lugha katika Mijadala Bungeni | 66 |
| 4.2.10 Hotuba kwa Wananchi Katika Lugha ya Kiswahili | 67 |
| 4.2.11 Uamuzi wa Kuchagua baina ya Kiingereza au Kiswahili katika Mazungumzo | 68 |
| 4.2.12 Hisia Chanya wakati wa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Bungeni | 69 |
| 4.2.13 Utazamaji Vipindi vya Televisheni katika Lugha ya Kiingereza | 70 |
| 4.2.14 Ujasiri wa kuzungumza Kiswahili | 71 |
| 4.2.15 Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili Fasaha | 72 |
| 4.2.16 Kiswahili ni Lugha inayohitaji Ufasaha kwa wingi | 73 |
| 4.2.17 Utazamaji wa Vipindi vya Televisheni katika Kiswahili..... | 74 |
| 4.2.18 Matumizi ya Kiswahili katika Mazingira ya Kazi | 75 |
| 4.2.19 Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Kitaifa | 75 |
| 4.2.20 Kiswahili kama Chombo cha Umoja wa Wakenya..... | 77 |
| 4.3 Hitimisho..... | 77 |
| SURA YA TANO | 79 |
| MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | 79 |
| 5.0 Utangulizi..... | 79 |
| 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti | 79 |
| 5.2 Vikwazo vya Utafiti | 84 |
| 5.3 Mapendekezo ya Mtafiti | 84 |
| 5.4 Hitimisho..... | 86 |
| MAREJELEO..... | 87 |
| KIAMBATISHO 1: FOMU YA IDHINI YA KUSHIRIKI KWENYE UTAFITI | 92 |

| | |
|--|------------|
| KIAMBATISHO 2: RAMANI YA JIMBO LA SIAYA NA BUNGE LA KAUNTI..... | 95 |
| KIAMBATISHO 3: BARUA YA IDHINI YA KAMATI YA MAADILI (ERC) | 97 |
| KIAMBATISHO 4: BARUA YA IDHINI(NACOSTI)..... | 98 |
| KIAMBATISHO 5: HOJAJI YA WAJUMBE WA BUNGE LA KAUNTI | 100 |
| KIAMBATISHO 6: MASWALI YA MAHOJIANO NA WAJUMBE WA BUNGE LA KAUNTI | 105 |



ORODHA YA VIELELEZO

| | |
|--|----|
| Kielelezo 1: Urahisi wa Kujifunza Kiswahili..... | 33 |
| Kielelezo 2: Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Kutoa Hoja Bungeni | 34 |
| Kielelezo 3: Uelewaji wa Ujumbe unaowasilishwa katika Kiswahili | 35 |
| Kielelezo 4: Dhima ya Kiswahili katika Maendeleo ya Taifa la Kenya | 37 |
| Kielelezo 5: Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari | 38 |
| Kielelezo 6: Matumizi ya Kiingereza katika Mijadala Bungeni | 39 |
| Kielelezo 7: Ugumu wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha Bungeni | 41 |
| Kielelezo 8: Athari za Makosa ya Kimatamshi katika Matumizi ya Kiswahili | 42 |
| Kielelezo 9: Kuchanganya Lugha wakati wa Kutoa Hoja Bungeni | 43 |
| Kielelezo 10: Utoaji Hotuba kwa Wananchi kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili..... | 45 |
| Kielelezo 11: Uamuzi wa Kuchangua Kutumia Lugha ya Kiingereza au Kiswahili. | 46 |
| Kielelezo 12: Ujasiri wa kutumia Lugha ya Kiswahili Bungeni | 47 |
| Kielelezo 13: Utazamaji Vipindi vya Televisheni katika Lugha ya Kiingereza | 49 |
| Kielelezo 14: Hisia za Unyonge wakati wa Kuzungumza Kiswahili..... | 50 |
| Kielelezo 15: Kutamani Ujuzi na Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili Fasaha..... | 52 |
| Kielelezo 16: Kiswahili ni Lugha yenye Ufasaha kwa Wingi..... | 53 |
| Kielelezo 17: Chuki katika kusikiliza Vipindi vya Televisheni kwa Kiswahili..... | 55 |
| Kielelezo 18: Matumizi ya Kiswahili Yanapaswa Kupigwa Marufuku Ofisini na Kazini | 56 |
| Kielelezo 19: Kiswahili ni Lugha Duni na isiyopaswa Kutumika Kitaifa | 57 |
| Kielelezo 20: Kiswahili ni Chombo cha Umoja wa Wakenya | 59 |

ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|--|----|
| Jedwali 2: Idadi ya Wawakilishi Wodi wa Jimbo la Siaya..... | 23 |
| Jedwali 3: Kiwango cha Mwitikio..... | 32 |
| Jedwali 4: Ni rahisi kujifunza Kiswahili | 60 |
| Jedwali 5: Napenda Kutumia Kiswahili Kutoa Hoja Zangu katika Mijadala Bungeni..... | 61 |
| Jedwali 6: Ninapotumia Lugha ya Kiswahili, Wajumbe Wenzangu Huelewa Ujumbe Vyema Zaidi | 62 |
| Jedwali 7: Lugha ya Kiswahili ina Dhima Kubwa kwa Maendeleo ya Taifa la Kenya..... | 62 |
| Jedwali 8: Kufurahia Vipindi Vinavyotolewa katika Kiswahili kwenye Vyombo vya Habari..... | 63 |
| Jedwali 9: Wanasiasa katika Kaunti Hupenda Kutumia Kiingereza katika Mijadala Bungeni..... | 64 |
| Jedwali 10: Ugumu wa Kuongea Kiswahili kwa Ufasaha | 65 |
| Jedwali 11: Matamshi ya Kiswahili yanaathiri Matumizi yake | 66 |
| Jedwali 12: Ninapotaka Wajumbe wanielewe vyema Wakati ninapotoa Hoja zangu Bungeni, mimi Hupenda Kuchanganya Lugha..... | 67 |
| Jedwali 13: Napenda Kuwahutubia Wananchi ninaowakilisha kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili . | 68 |
| Jedwali 14: Huchagua Kiswahili kila mara Ninapokabiliwa na Uamuzi wa Kuchagua Kutumia Lugha ya Kiingereza au Kiswahili | 69 |
| Jedwali 15: Hujihisi kuwa Shujaa Ninapotumia Kiswahili katika Mijadala Bungeni | 70 |
| Jedwali 16: Hupenda Kutazama Vipindi vya Televisheni katika Lugha ya Kiingereza | 71 |
| Jedwali 17: Nikiongea Kiswahili huwa Sijihisi Mtu Mnyonge..... | 72 |
| Jedwali 18: Ningepeda niwe na Ujuzi na Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha | 72 |
| Jedwali 19: Kiswahili ni Lugha yenye Ufasaha kwa wingi..... | 73 |
| Jedwali 20: Nachukia kusikiliza Vipindi vya Televisheni katika Kiswahili | 74 |
| Jedwali 21: Matumizi ya Kiswahili yanapaswa Kupigwa Marufuku kwenye Mazingira ya Kazini | 75 |
| Jedwali 22: Kiswahili ni Lugha Duni na Isiyopaswa Kulazimishwa Itumike Kitaifa..... | 76 |
| Jedwali 23: Kiswahili ni Chombo cha kuwaunganisha Wakenya..... | 77 |

VIFUPISHO NA AKRONIMU ZILIZOTUMIKA

VOA- Voice of America

BBC- Britain Broadcast Cooperation


Taz-Tazama

TUKI-Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

NACOSTI- National Commission of Science and Technology and Innovation

Uk-Ukurasa

UN- United Nations



SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii imefafanua usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vilevile mtafiti ameangazia sababu za kuchagua mada hii, umuhimu wa utafiti huu, upeo na mipaka ya utafiti wake pamoja na maelezo ya istilahi maalumu zilizotumika kwenye utafiti.

1.1 Usuli wa Mada

Lugha huwa chombo chenye umuhimu mkubwa sana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Ni chombo ambacho mwanadamu hutumia ili kuwasiliana na wenzake katika maisha yake ya kila siku. Richards na wengineo (1985) wanaeleza kuwa kuna aina mbalimbali za lugha zikiwemo lugha ya kitaifa, lugha rasmi na ile ya kimaeneo kutegemea majukumu ya lugha hiyo katika jamii. Wanaeleza kuwa lugha rasmi ni lugha iliyoteuliwa na serikali ya taifa fulani ili kutekeleza majukumu rasmi katika jamii. Majukumu hayo ni kama vile masuala ya utawala au uongozi, uchumi, biashara, elimu na masuala ya kimataifa kwa jumla.

Alivyofafanua Adegbiya (1994) ni kuwa mataifa mengi ya Bara la Afrika hutumia lugha za wakoloni kama lugha rasmi huku lugha zao asilia zikitumiwa katika mawasiliano na miktadha isiyokuwa rasmi. Msomi huyu anadai kuwa kuwa lugha nyingi asilia za Kiafrika hupewa hadhi ya chini huku zile za wakoloni zikitwikwa hadhi ya juu. Zaidi ya hayo, Adegbiya anaeleza kuwa hali hii imekuwa ikibadilika siku hadi siku katika miaka ya hivi karibuni na kufanya mataifa mengi ya bara hili kufanya lugha zao za Kiafrika kuwa lugha za kutumiwa kwenye mazingira rasmi. Uteuzi wa lugha ya kiafrika kuwa rasmi umeshuhudiwa katika taifa la Kenya ambapo lugha ya kiswahili imewekwa rasmi kwa mujibu wa katiba yake.

Katiba ya taifa la Kenya (2010) katika sura ya pili kifungu cha saba (ii) inabainisha kuwa, lugha

mbili; yaani, Kiingereza na Kiswahili zinatambuliwa kama lugha zinazoweza kutumiwa katika miktadha rasmi. Sura ya 8 kifungu cha 120 (v) inatambua lugha rasmi za bunge kuwa Kiingereza, Kiswahili na lugha ishara hivyo basi masuala ya bunge yanapaswa kuendelezwa kwa kutumia lugha mojawapo ya hizi tatu. Lugha ya Kiswahili ni lugha mojawapo ya Kiafrika ambayo imepewa hadhi ya juu sawa na lugha nyingine za wakoloni.

Kwa mujibu wa Kembo-Sure (1996), lugha ya Kiswahili ina muhimu katika maisha ya kila siku miongoni mwa Wakenya. Hii ni kwa sababu hii ndiyo lugha ya kitaifa na kuwa ndiyo inayojulikana kutoibua hisia zinazohusiana na ukabila miongoni mwa wazungumzaji wake. Wakenya wengi wamejifunga kibwebwe kujifunza Kiswahili kwani kinaashiria umoja wa kitaifa nchini. Lugha ya Kiswahili kwa mapana hutumiwa na watu wa makabila mbalimbali kama chombo cha mawasiliano. Lugha tukufu ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha nyingi za Kiafrika zilizotafitiwa na wasomi wengi wa bara la Afrika (Mbaabu, 1996). Kiswahili kimesambaa na kuzungumzwa pembe tofauti za Afrika Mashariki, kati na kusini zikiwemo mataifa ya Kenya, Tanzania, Uganda, Burundi, Rwanda, Msumbiji, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Visiwa vya Komoro na Afrika Kusini miongoni mwa pembe nyingine (Massamba na wenziwe, 2000:2).

Katika taifa la Kenya, Kiswahili hufundishwa wanafunzi kikiwa somo la lazima kwenye shule za msingi na vile vile shule za upili. Pia, lugha hii hufundishwa vyuoni vya Kenya ila hutahiniwa kama somo lisilo la lazima. Kadhalika, Kiswahili hutumika kwenye vyombo vya habari katika idhaa mbalimbali za redio na za runinga katika taifa la Kenya na pia kwenye idhaa za kimataifa kama vile Shirika la Kiswahili la Utangazaji la Uingereza (BBC) mjini London, Sauti ya Amerika (VOA) jijini Washington na pia Shirika la utangazaji la Ujerumani.

Zaidi ya hayo, katika taifa la Kenya, kuna mashirika yanayochapisha magazeti kwa kutumia Kiswahili kutolea kazi zao jinsi ilivyo kwa *Taifa Leo*. Lugha ya Kiswahili pia hutumiwa na wajumbe

bungeni wa bunge kuu la Kenya kwenye mijadala yake. Kwa kuwa na hadhi kubwa katika taifa la Kenya, Kiswahili hutumiwa kwenye mawanda ya kila siku ya kijamii yakiwemo yale ya biashara na ya kisiasa. Moseti mwaka wa (2002) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili hutumiwa na idadi pana ya wakenya kuwasiliana ikilinganishwa na lugha nyingine zote.

Chimera, 1998:1; anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo lugha sambazi inayoongoza huku ikizipiku lugha nyingi zinazozungumzwa eneo pana la Afrika Mashariki na Kati. Licha ya kuwepo na upinzani kutoka kwa lugha za kikoloni kama vile lugha ya Kiingereza na ya Kifaransa, Kiswahili kimesambaa pakubwa na kupanua nyanja zake hadi kufikia kiwango cha kukabiliana na lugha nyingine katika vilima vya kimataifa kwa kuengemea matumizi na majukumu yake.

Licha ya kuwa lugha ya Kiswahili ina umuhimu mkubwa na majukumu mengi, bado inakumbwa na pingamizi nyingi. Uchunguzi kuhusu matumizi yake unaonyesha kuwa hali yake bado haijafikia kiwango cha kuridhisha ulimwengu (Monachi, 2011). Baadhi ya vikwazo hivyo ni kuwepo kwa mielekeo mbalimbali ya lugha inayodhihirika katika jamii lugha za Wakenya. Haya ni kwa mujibu wa (Mukhwana, 2008)

Kwenye kongamano la sabini na sita la Muungano wa Umoja wa Mataifa Afrika mjini Durban nchini Afrika Kusini mwaka wa 2002, walipendekeza ukuzaji wa lugha za Kiafrika. Lugha ya Kiswahili ilitiuliwa kuwa lugha ambayo ingetumiwa katika mawasiliano kwenye kongamano hilo na pia walipendekeza iwe lugha ya mawasiliano Afrika nzima. Waliona haja ya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili katika masuala rasmi. Hali hii iliweza kuonyesha kuwa lugha ya Kiswahili siyo maarufu tu nchini Kenya bali Afrika nzima.

Kiswahili ni lugha ya Kimataifa inayozungumzwa kwenye pembe nyingi za Afrika Mashariki na ya kati. Lugha hii imetumiwa kwa muda wa miaka sabini tangu iliposanifishwa mwaka wa 1930. Hivi sasa ina hadhi ya lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Tanzania na Kenya. Pia ni somo la lazima

katika shule za msingi na shule za upili. Mara nyingi ikiwa nchi ina lugha rasmi mbili au zaidi, lugha hizo huwa na hadhi tofauti tofauti. Lugha rasmi moja inaweza kuwa na hadhi ya juu kuliko lugha rasmi nyingine na mambo mbalimbali huchangia hali hii ikiwemo mielekeo.

Kulingana na Su-Hie-Ting (2003), anasema kuwa mielekeo ya lugha katika jamii huzuka pale ambapo jamii ina lugha zaidi ya moja. Hali hii inadhahirika nchini Kenya kwani ina lugha rasmi mbili na wananchi wanaweza kuwa na mielekeo tofauti tofauti. Kulingana na Gaw (2008), mitazamo ya lugha huwa ni kipengele kikuu katika kujitambulisha na lugha. Anayezungumza lugha moja na zaidi huwa na mitazamo tofauti kuhusu lugha zote anazozungumza na mielekeo hiyo huathiriwa na vyeo vya lugha hiyo na mazingira yao.

Zaidi ya hayo, mielekeo ya watu hao hubadilika kulingana na umilisi wao wa lugha na mawasiliano katika lugha hiyo. Kwa muda mrefu, lugha ya Kiingereza imekuwa ndiyo lugha rasmi nchini Kenya na lugha ya Kiswahili imeweza kupewa hadhi hiyo ya kuwa lugha rasmi katika katiba ya Kenya (2010) (National Council for Law Reporting, 2010). Kwa hivyo lugha hizi mbili zitakuwa na mielekeo tofauti miongoni mwa wananchi.

Kulingana na Agheyisi na Fishman (1970), mielekeo yaweza kuwa tukio la kiakili au lisilofichika. Kwa kugemea tukio la kiakili, wanaeleza kuwa mielekeo husika ni ngumu kuonekana waziwazi na hivyo iwapo mtafiti angeweza kuelewa mielekeo ya watu hao kuhusu jambo fulani, ni lazima awasaili ama awahoji kuhusu dhana hiyo. Wanazidi kueleza kuwa mielekeo inahusu ujenzi wa makisio ambayo huhusiana moja kwa moja na tabia zinazodhahirika waziwazi.

Kwa kuzingatia hoja kuwa mielekeo ni tukio linalodhahirika waziwazi, wasomi hawa wanaeleza kuwa ili kuelewa mielekeo ya watu mtafiti hana budi kutazama na kunakili tabia za mtu katika jamii yake kupitia njia ya uchunzaji hasa anapotumia lugha husika kufanya mawasiliano na wanajamii wenzake.

Mielekeo hujengwa kutokana na hali inayomkumba binadamu katika maisha yake. Kwa mfano; kuzungumza, kusoma, kukua na kupata maarifa. Mielekeo vile vile hukua, hupungua na huimarika mtu anapozidi kuongeza maarifa katika shughuli mbalimbali. Mtu huchukua mwelekeo fulani na kushikilia mpaka anapobadili huo mwelekeo na kuchukua mwelekeo mwingine kuhusu jambo fulani kama asemavyo Sheriff (1965).

Watu hujenga mielekeo kuhusu mambo mbalimbali maishani. Kwa mfano watu huwa na mielekeo kuhusu siasa, uchumi, utamaduni, elimu, kati ya mengine mengi maishani. Wao hufanya hivyo kwa sababu tofauti tofauti kama vile, mielekeo husaidia mtu kubadilika kulingana na mabadiliko ya kilimwengu. Mtu hazaliwi na mielekeo bali hujenga kupitia maingiliano yake na sahiibu wake, jamii na hata pengine shuleni.

Utafiti huu ulizingatia mitazamo yote miwili katika kutathmini ile nafasi inayoongoza mielekeo ya uteuzi wa lugha inayotumika kwenye mijadala ya wabunge bungeni kaunti ya Siaya nchini Kenya. Mielekeo ya watu kuhusu mambo fulani kwa mara nyingi huweza kuathiri kitu au watu husika. Kwa kurejelea misingi hii, ni dhahiri kwamba mielekeo ya watu kuhusu lugha huweza kuwa na athari za jinsi watu hao huitazama lugha husika. Mitazamo kuhusu lugha hutokana na vichocheo fulani. Kufuatana na haya yote, mtafiti aliangazia nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha ya mijadala ya wajumbe bungeni katika kaunti ya Siaya. Kaunti hii ina wajumbe wa makabila mbalimbali kwa vile imepakana na majimbo ya Busia, Vihiga, Kakamega, Kisumu na vile vile taifa la Uganda. Sehemu hii ina makabila kadha; haya ni kama vile; wazungumzaji wa Dholuo, Kibaluha, Kihindi, Kisuba, Kinyore na kadhalika.

1.2 Suala la Utafiti

Katiba ya Kenya (2010) inapatia lugha ya Kiswahili hadhi ya kuwa lugha rasmi kinyume na hapo

awali. Halikadhalika, lugha hii kupitia tume ya Gachathi (1979) Kiswahili kilifanywa cha lazima na cha kutahiniwa shuleni na haswa za msingi na za sekondari. Kwa hivyo, matarajio na mitazamo kuhusu majukumu ya Kiswahili yamebadilika na hii huenda ikaathiri au kuathiriwa na mielekeo ya watumizi wa Kiswahili katika shughuli mbalimbali ikiwemo za kielimu, siasa, dini, biashara na utamaduni. Mikadha rasmi ya matumizi ya Kiswahili ni pamoja na ile ya shughuli za bunge la kitaifa pamoja na mabunge arobaini na saba (47) ya ugatuzi kulingana na katiba ya 2010. Mabunge haya hubidi kutumia lugha zinazoeleweka na wananchi wote kwani sheria zinazotungwa huwa mwongozo wa wananchi kwa jumla. Wajumbe wanapokutana bungeni, huongozwa na mielekeo kuteua lugha watakayotumia katika mijadala bungeni kati ya zile zilizoidhinishwa kutumika. Hata hivyo, haijulikani ni mielekeo ipi walio nayo wajumbe kuhusu lugha zinazotumika katika mijadala ya bunge jambo ambalo lilichunguzwa katika utafiti huu. Aidha, utafiti ulichunguza sababu zinazowapelekea wajumbe kuteua lugha moja dhidi ya nyingine kati ya zile wanazotumia katika mijadala bungeni.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu ambalo linafafanuliwa na malengo mahususi. Malengo haya yamejadiliwa katika sehemu inayofuata:

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kubainisha ikiwa mielekeo ya wazungumzaji kuhusu lugha inachangia uteuzi wa lugha wanayotumia katika mijadala ya wajumbe bungeni katika kaunti ya Siaya nchini Kenya.

1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti

Malengo mahususi yaliyozingatiwa kwenye utafiti huu yalikuwa yafuatayo:

- i. Kuchunguza ikiwa mielekeo ya wazungumzaji kuhusu lugha ina mchango wowote kuhusu uteuzi wa lugha wanayotumia katika mijadala bungeni katika kaunti ya Siaya.
- ii. Kuchanganua sababu zinazowachochea wajumbe wa serikali ya Kaunti ya Siaya kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine katika mijadala yao bungeni.
- iii. Kubainisha iwapo kuna lugha mahususi inayopendelewa na wajumbe katika mijadala yao bungeni katika kaunti ya Siaya.
- iv. Kuchunguza iwapo kuna pingamizi zinazowazuia wajumbe wa Kaunti ya Siaya kutumia Kiswahili kufanikisha mawasiliano katika muktadha wa mijadala bungeni.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo ya utafiti:

- i. Je, mielekeo ya wazungumzaji kuhusu lugha ina mchango gani katika uteuzi wa lugha wanayotumia kwenye mijadala bungeni katika kaunti ya Siaya?
- ii. Ni sababu zipi zinazowachochea wajumbe wa serikali ya Kaunti ya Siaya kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine katika mijadala yao bungeni?
- iii. Je, kuna lugha mahususi inayopendelewa na wajumbe katika mijadala yao bungeni katika kaunti ya Siaya?
- iv. Ni pingamizi zipi zinazowazuia wajumbe wa Kaunti ya Siaya kutumia Kiswahili kufanikisha mawasiliano katika muktadha wa mijadala bungeni?

1.5 Sababu za Kuteua Mada

Baada ya ukoloni, serikali ya Kenya imekuwa ikiteua tume mbalimbali kama vile; zile za Ominde (1964), Gachathi (1976), Mackay (1981) kuchunguza masuala ya elimu nchini Kenya. Tume hizi zimekuwa zikitoa mapendekezo kuhusu lugha zinazopaswa kutumiwa katika sekta ya elimu na mapendekezo hayo yameweza kutekelezwa. Hali hii ya kuwa na sera za lugha zinazohusiana na

elimu pekee yake na wala sio wizara ni mojawapo ya sababu ambayo ilichangia uchaguzi wa mada hii.

Shughuli nyingi rasmi nchini huendelezwa na kutekelezwa katika wizara za serikali na lugha ndiyo kifaa chenye umuhimu mkubwa na kinachotumiwa kwa kuwasiliana ili kutoa na kupokea huduma kati ya wanasiasa na wananchi. Utafiti uliofanywa basi umebainisha mielekeo ya viongozi wa kisiasa kuhusu lugha wanayotumia katika mawasiliano ya kiserikali wanapojadiliana bungeni katika kaunti ya Siaya. Mielekeo kuhusu lugha imebainisha umuhimu wa Kiswahili na Kiingereza katika mawasiliano ya kisiasa.

Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi mpya ya kuwa lugha rasmi katika katiba ya Kenya (2010) na Wakenya hawana budi kuifahamu na kuitumia katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. Utafiti huu ulinuia kuonyesha ikiwa wajumbe katika serikali za kaunti wana umilisi wakutosha katika Kiswahili ili kuitumia katika mawasiliano yao wanapokuwa bungeni. Hali hii itahimiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kiserikali na utoaji huduma kwa wananchi katika wizara mbalimbali za serikali katika Kiswahili.

Sababu nyingine ilikuwa ni kutathmini ikiwa mapendekezo yaliyomo katika katiba ya mwaka wa (2010) kuhusu lugha yalitekelezwa vilivyo na wananchi hasa kule vijijini. Kellman mwaka wa (1971) akinukuliwa na Adegbija mwaka wa (1994) anasema wananchi wengi barani Afrika walio vijijini wakati mwingi hawajui kinachoendelea katika wizara za serikali hasa mijadala ya wajumbe bungeni kwa sababu lugha za kiafrika hazitumiwi. Hali hii imewafanya wengi wasichangie vikamilifu katika masuala ya taifa yanayohusiana na nchi yao na pia kutopokea huduma wanavyotaka katika lugha wanayoelewa.

Gaw mwaka wa (2008) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha iliyojikuta katikati mwa lugha

za Kienyeji na lugha ya Kiingereza na pia ni lingua franca ya Afrika Mashariki. Hali hii inaonyesha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika iliyoenea sana nchini Kenya kuliko lugha nyingine za Kiafrika. Wananchi wengi nchini Kenya wanaweza kujieleza vyema kwa kutumia lugha hii ya Kiswahili haswa vijijini hivyo basi, utafiti huu unataka kuonyesha ikiwa kuna uwezekano kuwa kuna lugha mahususi inayopendelewa na wajumbe katika mijadala yao bungeni na ikiwa wajumbe hao wana sababu maalum zinazowapeleka kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine katika mijadala yao bungeni katika kaunti ya Siaya.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Lugha tofauti zimekuwa zikichaguliwa na mifumo tofauti ya uongozi ili kutumika katika mifumo yao ya uongozi na hasa hali iliyo na urasimi. Kuna vitegemezi vingi ambavyo huchangia uteuzi wa lugha zinazopaswa kutumiwa na viongozi na wananchi wa jamii fulani. Mielekeo tofauti imekuwa ikijikita kwenye mifumo tofauti ya kisiasa huku wajumbe ambao wametwikwa majukumu ya kutunga sheria za kuongoza jamii fulani ya watu. Kwa kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano miongoni mwa jamii ya mwanadamu, hamna budi kuwa ni mwelekeo utakaolenga kujenga maadili miongoni mwa jamii ya kesho. Kwa vile taifa la Kenya lina makabila yenye lugha, tamaduni na imani tofauti ni lazima kila jimbo kuibuka na msimamo dhabiti kuhusu lugha itakayotumika kwenye shughuli rasmi za kujenga utangamano wa kijamii.

Mtafiti alijikita kwenye matumizi ya lugha ya kisiasa kwenye kaunti ya Siaya yenye makabila tofauti na hivyo basi mapendekezo yaliyotolewa yatasaidia viongozi wa kisiasa kwenye jimbo hili kuwa na misimamo isiyoterereka kuhusu mielekeo ya lugha itakayotumika kwenye bunge lao ili kujenga uwiano wa makabila tofauti yanayopatikana katika jimbo hili. Nafasi inayoongoza mielekeo wakati wa kuteua lugha inayotumika kwenye mijadala ya wajumbe ni suala pana ambalo halijashughulikiwa na hivyo basi mtafiti alinuia kuziba pengo lililopo kwenye suala hili nyeti la kisiasa.

1.7 Mawanda na Mipaka ya Utafiti

Katiba ya Kenya 2010: sura ya 11 kifungu cha 2 (i), inaeleza kuwa nchi ya Kenya, imegawanywa katika serikali za kaunti. Nchini Kenya, kuna kaunti arubaini na saba na ile ya Siaya ni mojawapo yake. Utafiti unatarajiwa kufanyika kaunti ya Siaya kwa sababu ina wajumbe wa serikali kutoka maeneo na makabila mbalimbali kwa kujipata kwenye mpaka wa Kenya na Uganda.

Zaidi ya hayo, katiba ya Kenya imewapa Wakenya haki ya kuishi na kufanya kazi katika kaunti yoyote ikiwemo Siaya. Wizara mbalimbali zitateuliwa katika utafiti huu kwani zina ukuruba zaidi na wananchi pamoja na wajumbe wa maeneo haya ya Siaya. Utafiti huu uliwalenga wajumbe walioteuliwa kuwakilisha wodi mbalimbali katika bunge la kaunti ya Siaya nchini Kenya.

1.8 Maelezo ya Istilahi Maalumu zilizotumika

Lugha- Lugha ina maana ya mfumo unaotumia sauti zenye unasibu unaoweza kutumiwa na watu wa jamii fulani iliyojikita kwenye tamaduni zake kwa minajili ya kuwasiliana.

Gatuzi- Hili ni eneo la utawala lenye kufuata mfumo wa uhawilishaji wa madaraka na ugavi wa matumizi ya rasilimali kutoka serikali kuu kwenda kwa serikali ndogo, lenye kuongozwa na gavana.

Bunge- Ina maana ya mkusanyiko wa vyombo vinavyotumiwa kwenye utungaji wa sheria kwenye utawala fulani wa jamii.

Siasa- Hii huwa na maana ya mbinu fulani inayotumiwa na jamii kwa minajili ya kufanya maamuzi fulani ya kugawana rasilimali za jamii hiyo.

Mielekeo- Hizi ni hisia walizo nazo watu kuhusu lugha fulani na ambazo hujengwa kiwakati kutokana na tajriba ya wanaohusika nayo na ambayo huathiri vitendo vya mtu.

Wajumbe- Hawa ni watu ambao huwakilisha wengine katika shughuli fulani. Ni wabunge

Katiba- Huu ni mfumo wa sheria unaoainisha misingi mikuu ya kisiasa na kuonyesha madaraka na majukumu ya serikali.

Lugha rasmi- Hii ni lugha iliyoteuliwa na kupewa cheo na uongozi fulani wa serikali ili kutumika katika shughuli zenye urasimi wa ofisini.

Mijadala-Haya ni mazungumzo juu ya mambo maalumu yanayofanywa kwa kutolea hoja jambo hilo.

Hoja- Haya ni maelezo yenye misingi na vigezo yanayotolewa kuthibitisha ukweli au uhalali wa jambo na pengine kupinga maelezo ya hapo awali.



SURA YA PILI

MWAUO WA MAANDISHI

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti aliangazia maandishi tofauti yanayohusiana na mada yake. Kazi hizi tangulizi zilikuwa na umuhimu mpana kwani zilimwelekeza mtafiti au mchunguzi kupekua taaluma iliyofichwa na kutambua pengo lililopo kwenye kazi yake. Katika kutekeleza jambo hili ilibidi mtafiti kusoma majarida, magazeti, vitabu, tasnifu, mitandao na maandishi yoyote yale yaliyo na uhusiano na mada ya mtafiti. Kulingana na Masasa mwaka wa (2017) kazi tangulizi pia hutoa ujuzi na maarifa ya waliowahi kufanya kazi zenye uhusiano na kazi ya mtafiti. Vile vile kwenye sura hii mtafiti aliangazia misingi ya nadharia zilizotumika katika mchakato mzima wa utafiti.

2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Huku akiangazia mielekeo ya lugha, Furaha (1991) alieleza namna mielekeo inavyoathiri uteuzi wa lugha ya matumizi ya siku baada ya siku miongoni mwa wakaaji wa Malindi. Utafiti wa Furaha umebaini kuwa katika mchakato wa kuteua lugha ya matumizi ya wakaaji wa Malindi, hujikita kwenye mielekeo ambayo huwa nayo wazungumzaji wale kuhusu lugha mbalimbali zinazopatikana kwenye eneo hili. Utafiti wa Furaha ulijikita kwenye lugha nne zinazopatikana miongoni mwa wakaaji wa Malindi; Kiswahili, Kijerumani, Kiingereza na Kiitaliano. Utafiti huu ulibaini kuwa Wanamalindi huenzi Kitaliano kwa kiasi kikubwa na kufuatwa na Kiswahili huku wakaaji hawa wakiwa mielekeo hasi kuhusu lugha asilia za mama kwenye mji huu wa Kaskazini mwa Pwani. Utafiti wa Furaha ulimjengea mtafiti msingi bora kwa kulinganisha mielekeo ya lugha ila Furaha alijikita kwenye mawasiliano ya wazungumzaji kwa jumla kinyume na mtafiti aliyelenga kubaini mielekeo hii tu kwa wajumbe kwenye bunge teule la Siaya.

Adegbija (1994) katika alichunguza mielekeo ya lugha za wakaazi wa mataifa ya Afrika zikilinganishwa na lugha za kikoloni alifafanua kuwa nchi nyingi za Afrika na haswa yanayopatikana eneo la ukanda wa jangwa la sahara zina mielekeo chanya kuelekea lugha za kikoloni huku zikilinganishwa na lugha asilia za Afrika. Licha ya hayo, Adegbija anaeleza ya kwamba baadhi ya jamii chache za Afrika zimekana lugha za kikoloni na kuheshimu lugha zao asilia kwa dhati. Hata hivyo mwandishi huyu analalama kuwa lugha za jamii hizi zilizodumisha utamaduni wao kwa muda mrefu hazijafanyiwa utafiti wa kutosha. Utafiti huu ulimfaa mtafiti kwa kujenga misingi yake kwenye mielekeo ya lugha asilia za kiafrika na zile za kigeni ila utofauti uliopo ni kuwa mtafiti alinulia kukita kambi yake kwenye uwanja wa mijadala kwenye bunge la kaunti teule kutafuta kupata ukweli wa iwapo kuna misukumo inayochochea wajumbe kuwa na mielekeo fulani ya uteuzi wa lugha wakati wa mijadala yao bungeni.

Thiba (2000) kwenye utafiti wake uliojikita nchini Afrika Kusini kuchunguza historia ya sera ya lugha na milelekeo yake iliyoibuliwa na sera za lugha, anadai kuwa wakati wa ukoloni, sera za wazungu zilipandisha vyeo lugha za Kiafrika na Kiingereza na kuzifanya lugha za ofisini au rasmi. Hali hii ilipingwa kwa dhati na Waafrika asilia kule nchini Afrika Kusini na hali hii ikazalisha maadamano ya kihistoria yaliyoongozwa na walimu na wanafunzi kupinga sera hizi kadamizi. Kilele cha maandamano haya kilizaa matunda matamu Afrika Kusini kwani mkoloni alibadili sera asilia na kuruhusu kuwepo kwa baadhi ya lugha za Kiafrika kama lugha rasmi zikiwemo isiZulu, isiXhosa, isiNdebele siSwati miongoni mwa lugha nyingine za Kiafrika. Kazi hii ya Thiba ilijenga msingi bora kwa kazi ya mtafiti kwani ilifafanua mielekeo ya jamii ya Afrika kuhusu lugha zisizokuwa na mashiko kwao. Mwanja uliopo kwa kazi hii ni kuwa haijajikita kwenye uongozi wa bungeni kunakotungiwa sheria na hivyo basi mtafiti alinulia kuziba mwanja huu kwa kufanyia utafiti mielekeo ya lugha iliyojikita kwenye bunge la kaunti teule.

Katika kazi ya Muthwii na Kioko (2001), walitafitia mielekeo ya Kiingereza cha aina tatu; kinachotumiwa na Wakenya; Kiingereza cha Uingereza, Kiingereza cha Wakenya na Kiingereza ‘Sanifu’. Wasomi hawa walibaini kuwa Kiingereza kinachoenziwa na Wakenya wengi ni Kiingereza Standard kilichosifika vijijini na mijini kwa sababu ndicho kilichotumika kwenye maofisi mengi na watumishi wa umma kama lugha rasmi. Kazi ya Kioko na Muthwii ilikuwa na msingi bora kwa mtafiti kwani inalinganisha mielekeo ya jamii kwenye lugha tofauti kwa jumla. Mwanja uliopo kwa kazi yao ni kuwa hawajaangazia masuala ya bungeni ambayo mtafiti alikusudia kutafitia ili kubaini vipengele vinavyowasukuma wajumbe kuwa na mwelekeo fulani kuhusu lugha ya mijadala yao.

Tasch (2003) katika utafiti wake uliotafitia kuhusu mielekeo ya lugha ya matumizi katika elimu nchini Uganda, alieleza Kiingereza ndiyo inayopewa kipao mbele na wengi wanaoshughulika na ufunzaji wa wanafunzi shuleni licha ya kuwa na Kiganda, Kiswahili pamoja na lugha zingine za asilia. Katika utafiti wake, Tasch anatambua kuwa wazazi wengi nchini Uganda wanaenzi na wana mielekeo chanya kuelekea lugha zao asilia kwa sababu kulingana na historia na utamaduni zao lugha hizi ndizo walizotumia katika malezi ya watoto wao. Utafiti huu ulionyesha kuwa Wanabaganda wengi walichukia lugha ya Kiswahili kwa hofu kuwa ingeleta ushindani kwa lugha yao ya Kiganda iliyosheheni hifadhi za utamaduni wao asilia. Hata hivyo, kwa vile lugha ya Kiswahili ina hadhi pana Afrika ya Mashariki, jamii nyingine pale Uganda zilieni lugha hii ya Kiswahili. Kazi ya Tasch ilimfaa mtafiti kwa kujikita kwenye mielekeo ya uteuzi wa lugha kwenye sekta muhimu ya elimu ila tu mtafiti aliepukana na masuala ya shuleni na kukita kambi kwenye bunge teule ili kubaini vichocheo vya wajumbe kuhusu lugha waliyoenzi katika mijadala yao pale bungeni.

Batibo (2005) katika utafiti wake anadai ya kwamba suala linalohusu mielekeo kuhusu lugha ni

hali ya kawaida tu miongoni mwa wanajamii. Anaeleza ya kwamba suala linalohusiana na mielekeo inayohusu lugha kwa mapana haliwezi kukosekana miongoni mwa wanajamii walio na lugha mosi au wingi lugha na mielekeo wa lugha huelekea sehemu moja kuhusu ile lugha ya jamii inayotumia lugha moja na mara nyingi mwelekeo huo huwa chanya. Vile vile, hali ya mielekeo fulani kuhusu lugha hudhihirika kutokana na vyeo ambavyo vimeambatanishwa na zile lugha tofauti kwa jamii ambazo hutumia lugha zaidi ya moja. Utafiti wa Batibo japo ulikuwa wa manufaa makubwa kwa mtafiti kwa kuangazia ulinganifu uliopo kwenye mielekeo ya lugha kwa jamii zinazotumia lugha moja na zile zinazotumia lugha nyingi, ulikuwa na tofauti na aliokusudia kufanya mtafiti kwani wake ulijikita kwenye mijadala ya bungeni kuchunguza ni vipi mielekeo inachangia uteuzi wa lugha wakati wa mijadala kwenye bunge teule.

Ennaji (2005) huku akitafitia suala la mielekeo kuhusu lugha katika taifa la Moroko kwa kurejelea lugha za Kiarabu cha Ustandard, kile Kiarabu cha Wamoroko na Kifaransa anaeleza ya kwamba Wamoroko wengi wana mielekeo iliyo chanya kuhusu Kiingereza kwa kukiona kama kiunganishi cha mawasiliano kati yao na mataifa mengine ya ulimwengu. Kulingana na Ennaji, lugha za Kifaransa na Kiarabu-kistandard zimepewa hadhi ya juu kimatumizi licha ya kuwa Kiarabu cha Morocco ndiyo lugha asilia iliyosheheni uhifadhi wa tamaduni za Waafrika asilia kutoka Morocco. Mwanja uliopo kwa kazi ya Ennaji ni kuwa licha ya kuwa na msingi bora kwa mtafiti kwa kuangazia mwelekeo wa lugha haijaangazia masuala ya wajumbe na mijadala yao bungeni bali imeangazia mielekeo ya uteuzi wa lugha kwa serikali na wananchi kwa jumla. Mtafiti alikusudia kuziba mwanya huu kwa kuangazia mielekeo inayochochea wajumbe kuteua lugha fulani wakati wa mijadala yao.

Muaka (2009) kwenye utafiti wake ameangazia kuhusu mielekeo ya lugha kwa vijana nchini Kenya. Huku akishughulikia mielekeo ya vijana kuhusu lugha katika miji ya Nairobi na

Kangundo inayoegemea Kiingereza, Kiswahili pamoja na lugha asilia ikiwemo Kikamba na namna mielekeo yake hutegemea sera zilizowekwa katika taifa la Kenya, Muaka ameonyesha jinsi sera hizi zinavyoathiri matumizi ya lugha fulani miongoni mwa vijana. Kulingana na Muaka, sera ya lugha ya Kiingereza kupewa hadhi ya juu kama lugha rasmi ofisini, ni hali ambayo imefanya baadhi ya vijana waliomo mijini na kwenye vijiji wawe na mielekeo iliyo na uchanya wa lugha hii ya kikoloni. Vile vile, vijana hawa huwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na lugha za mama. Kazi ya Muaka ilimfaa mtafiti kwa vile imetafitia mielekeo ya lugha miongoni mwa watumizi wake. Tofauti iliyopo ni kuwa Muaka alitafitia vijana lakini mtafiti alitafitia wajumbe na kazi yao ya mijadala kwenye bunge teule.

Babusa (2010) alilinganisha mitazamo ya wanangezi walio shule za upili inayohusu Kiswahili na jinsi mitazamo husika huathiri uwezo wa kuwa na umilisi wa lugha kwa wanafunzi hawa kwenye mikoa ya Nairobi na Mombasa. Kwenye utafiti wake Babusa, inabainika kuwa wale wanangenzi wanaopatikana Pwani ya Kenya wana falsafa chanya kuengemea Kiswahili wakilinganishwa na wanaopatikana katika jiji la Nairobi. Pia, Babusa alibaini ya kwamba wanafunzi wa jinsia ya kike wana tajriba ya juu wa lugha ya Kiswahili huku wale wa kiume wakiwa na umilisi wa kiwango cha chini kwani viwango vya mielekeo yao ilitofautiana pia. Utafiti wa Babusa ulijenga msingi bora kwa kazi ya mtafiti kwa kuweka msingi bora kuhusu mwelekeo wa lugha. Mwanja uliopo na ambao mtafiti anakusudia kuziba ni kuwa Babusa alijikita kwenye mielekeo ya lugha miongoni mwa wanafunzi shuleni lakini yeye alijikita kwenye masuala ya siasa kwa kuangazia wajumbe kwenye bunge teule ambalo ni bunge la Siaya.

Nyandwaro (2015) alifanya utafiti kuhusu mielekeo ya wafanyi kazi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi katika wizara za serikali nchini Kenya. Kulingana na Nyandwaro, lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa katika sekta mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo nchini Kenya

zikiwemo sekta za elimu, siasa na kwenye vyombo habari. Mtafiti huyu anadai mwelekeo wa serikali kuteua lugha hii kwenye nyanja hizi, wananchi watakuwa na nafasi ya kuungana pamoja kwani ni lugha rahisi kueleweka na hivyo basi maendeleo yataafikiwa bila ugumu mwingi. Kazi ya Nyandwaro ilimfaa mtafiti kwani ilijikita kwenye mwelekeo wa uteuzi wa lugha miongoni mwa watumishi wa umma. Tofauti iliyopo na utafiti aliokusudia kufanya mtafiti ni kuwa utafiti wake haukulenga wafanyikazi wa serikali kwa jumla bali ulijikita kwenye majengo ya mabunge teule kwa kuengemea masuala ya mijadala inayofanywa na wajumbe ili kubaini iwapo mielekeo ilichangia uteuzi wa lugha, iwapo kuna lugha mahususi iliyopendelewa na wajumbe, iwapo wajumbe wana sababu maalumu zilizowapelekea kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine na iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia wajumbe kutumia kiswahili kufanikisha mawasiliano wakati wa mijadala yao kwenye bunge lao.

Kwa kuangazia kazi mbalimbali zilizoandikwa na waandishi tofauti kuna idhibati kuwa bado kuna mwanya uliohitaji kujazwa kuhusu mielekeo ya lugha. Ingawa kazi maridhawa zimeshughulikia mielekeo kuhusu uteuzi wa lugha, kazi hizi hazijashughulikia mielekeo ya lugha hizi kwa kuegemea suala nyeti la siasa na haswa zile za magatuzi. Hivyo basi mtafiti alikita kambi kwenye mielekeo hii ya uteuzi wa lugha ya mijadala ya wajumbe bungeni kwenye kaunti moja teule; kaunti ya Siaya.

2.2 Misingi ya Nadharia

Nadharia ni neno linalotumiwa kurejelea kauli fulani au faida zinazotegemezwa kwenye uwazaji wa aina fulani. Pia ni mfumo wa mawazo yanayoeleza kuhusu maisha ya mwanadamu na mazingira yake (Wamitila, 2003). Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili zifuatazo:

2.2.1 Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa

Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa ambayo iliasisiwa na Ajzen na Fishbein (1980) inadai kuwa

binadamu ni kiumbe mwenye urazini tofauti na viumbe wengine wenye uhai na anaweza kuratibu chochote kile kwa kutumia maarifa aliyo nayo. Waasisi hawa wanapingana na madai kuwa tabia ya binadamu inadhibitiwa na nia na kueleza ya kwamba mwanadamu huyu hutabiri athari ya matendo yake kabla ya kuamua kujihusisha ama kutekeleza tabia anayokusudia. Waasisi hawa wanadai kuwa ikiwa binadamu ana nia ya kufanya jambo ambalo litamnufaisha atakuwa na mtazamo unaokubalika kuhusu jambo hilo na labda ikiwa jambo lile halitakuwa na faida kwake basi mtazamo wake utakana jambo lile. Kusudi kuu la nadharia hii ni kutabiri na kuwa na ufahamu na tabia ya mtu hata kabla ya kutekelezwa kwa ile tabia.

Mihimili ya Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa ni hii ifuatayo:

- i. Nadharia hii hutabiri na kuelewa tabia za watu ambapo kabla ya kuzielewa tabia hizi ni lazima mtu atathmini kinachosababisha tabia hizo. Waasisi hawa wanaeleza kuwa hakuna uzito kutabiri tabia za binadamu ila wakati mwingine kutokana na matukio yasiyotabiriwa binadamu huyu anaweza kubadili tabia iliyotarajiwa.
- ii. Nadharia hii inasisitiza kuwa nia ya mtu mara kwa mara hutathminiwa na vipengele vya kimsingi ambavyo ni;
 - a) Mielekeo ya mtu aliyo nayo kuhusu kitendo, imani yake kuhusu kitendo anachokusudia kutekeleza na pia tahmini yake inayohusiana na kitendo anachokusudia kutekeleza.
 - b) Kinachotarajiwa na mtu au watu na kinachohusiana na kitendo kilichotendwa.
 - c) Kusudi la utendaji ambalo mara nyingi hutokana na ule uchochezi alio nao mtu fulani wa kutekeleza kitendo na unaojikita kwenye mielekeo kuhusu jambo na pia kinachotarajiwa na wengine kuhusu utekelezaji wa jambo hilo.

Katika kipengele kilicho na msingi wa ubinafsi wa mtu ni kuwa binadamu yeyote hutathmini kwanza ikiwa tabia anayokusudia kuwa nayo itampa faida na ikiwa ni kweli itamnufaisha basi atakuwa na mwelekeo bora kwake na ikiwa haitampa faida yoyote basi binadamu huyu anakuwa na mwelekeo hafifu. Moja kwa moja huu ni mwelekeo kuhusu tabia. Kwa upande wa kipengele kilichojikita kwenye msingi wa ushawishi wa jamii inayomzunguka mtu, binadamu atakuwa na mtazamo bora ikiwa tabia yake itakuwa na ukubalifu katika jamii yake lakini ikiwa ile tabia yake itakuwa na matokeo ovyo kwenye jamii yake basi binadamu huyu atakuwa na mtazamo hafifu kuitekeleza. Hii ina maana kuwa kabla ya kutekeleza tabia yoyote, binadamu hujiuliza swali iwapo matendo yake yatamfaidi au yatafaidi jamii yake au la na ikiwa hayatakuwa na faida yoyote anayatupilia mbali.

Kwa jumla binadamu ataamua kufanya vitendo vinavyokubalika na jamii yake na haswa iwapo amepewa cheo fulani katika jamii anamotoka. Waasisi hawa wanaeleza kuwa ili utambue ikiwa mielekeo ya mtu ni chanya au hasi, ni lazima upime tabia ya mtu huyo kwa kumhoji moja kwa moja au kumpa jojaji ajaze ili kusoma kilicho kwenye akili yake kwani tabia yoyote ile hujengwa ndani ya akili kabla ya kutekelezwa.

Mpangilio wa nadharia hii umejijenga kwa kinachotarajiwa na mtu kuhusu matokeo ya kitendo chake, mielekeo inayohusiana na kitendo au mienendo, matarajio ya wengine kuhusu kinachokusudiwa kutendwa, nia ya kutekeleza kitendo husika na kisha kuwa na maamuzi ya kutekeleza kitendo au tabia au kuitupilia mbali.

Mihimili ya nadharia hii ilikuwa na faida kwa mtafiti kuafikia lengo la kwanza na la pili kwa kuchunguza iwapo mitazamo, mielekeo na matarajio fulani ya kibinafsi au ya kijamii inachangia uteuzi wa lugha inayotumika katika mijadala ya wajumbe bungeni na kuangazia iwapo wajumbe wa serikali wana sababu maalumu zinazowapelekea kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine

katika mijadala yao katika kaunti ya Siaya. Hii ni kwa sababu mielekeo yoyote ile wanayogemea kuteua lugha fulani itakuwa na athari zake kwao wenyewe na kwa jamii iliyowatunukia nafasi ya kuwa na vyeo na mamlaka walio nayo.

2.2.2 Nadharia Jumuishi ya Utambulisho

Nadharia hii iliasisiwa na Howard Giles mwaka wa 1982. Giles mwaka wa (1982) anaeleza kuwa kuna maingiliano ya lugha kwa misingi ya unenaji, ishara na maandishi. Mawazo makuu ya nadharia hii yanaweza kusawiriwa kwa njia tofauti kama vile; watu wanapoingiliana wanabadilishana usemi, sauti na ishara ili kujihusisha na wengine. Pili, nadharia hii inasisitiza mahusiano kati ya lugha, muktadha na utambulisho ambapo kuna ujihusishaji wa aina mbili; ule wa makutano na ule wa mwachano. Kulingana na Giles, makutano ni namna ambavyo watu hubadili usemi, ishara na sauti ili kujumuisha washirika wao katika mawasiliano kwa lengo la kupunguza tofauti baina yao na kudhihirisha ujihusishaji wao. Giles anaeleza kuwa watu wanaweza kuwa na makutano kupitia njia mbalimbali zikiwemo matumizi ya lugha, matamshi, sauti na hata tabia zisizo za usemi.

Kulingana na nadharia hii, sio lazima watu wajihusishe katika mambo husika wakati mmoja bali wanaweza kuwa na makutano kwa kiwango kimoja na kuwa na mwachano katika viwango vingine. Mtu anaweza kwa nafsi yake kujinyima kitu fulani kwa faida ya washirika wake ili naye afaidike kwa kujihusisha na wale anaowasiliana nao. Kulingana na Turner na Richard mwaka wa (2010), Kuna mambo yanayoweza kusababisha kuleta makutano ambayo ni kama vile;

- i. Kufanana kwa utamaduni
- ii. Kuoana kwa matumizi ya lugha
- iii. Maingiliano tarajiwa
- iv. Hadhi

- v. Historia
- vi. Kaida
- vii. Mamlaka
- viii. Matamano ya kibinafsi

Nadharia hii ilimfaidi mtafiti kuafikia lengo la tatu na la nne ambayo haswa yalijengeka katika misingi ya mahusiano na ujihusishaji. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza iwapo kuna lugha mahususi inayopendelewa na wajumbe wa kaunti ya Siaya katika mijadala yao bungeni. Hii ni kwa sababu wajumbe hawa wanapokutana ni lazima wahusiane kwa karibu na kupendelea lugha wanayoimudu ili watekeleze majukumu na matakwa ya waliowachangua. Vile vile nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchunguza iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia wajumbe wa kaunti ya Siaya kutumia lugha ya Kiswahili kufanikisha mawasiliano katika muktadha wa mijadala bungeni. Hii ni kwa sababu hata kama wengi wa wajumbe hawa ni wa jamii za Waluo kuna lahaja mbalimbali ndani mwa jamii hii zilizo na matamshi yanayoweza kukinzana na matamshi bora ya Kiswahili sanifu.

2.3 Hitimisho

Katika sura hii ya pili, kazi tangulizi kuhusu mada ya mtafiti zimejadiliwa pamoja na kujadili misingi ya nadharia ambazo zilitumika na mtafiti katika utafiti wake. Nadharia hizi zilikiwa ni pamoja na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa pamoja na ile ya Jumuishi ya Utambulisho.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na uteuzi wa sampuli, mbinu na vifaa vya kukusanya data, maadili yaliyoongoza utafiti na kisha uchambuzi na uwasilishaji wa data iliyopatikana.

3.1 Muundo wa Utafiti

Kulingana na Renatus mwaka wa (2017) muundo wa utafiti ni mpangilio wa taratibu zinazotumika kukusanya au kuchambua data kwa namna inayounganisha data zilizopatikana na malengo ya utafiti. Muundo wa utafiti wenyewe ni uchunguzi wa kinathari na ambapo matokeo yake yataandikwa kwa lugha ya kinathari. Katika utafiti huu mtafiti alitembelea maktaba za vyuo vikuu vya Maseno, Jaramogi Oginga Odinga na chuo kikuu cha Mount Kenya. Katika mchakato mzima wa utafiti, mtafiti alidurusu maandishi mbalimbali na tasnifu zilizohusiana na jamii pana ya Waluo ambapo jimbo la Siaya hupatikana.

3.2 Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa Creswell mwaka wa (2009), eneo la utafiti ni mahali ambapo kazi halisia ya utafiti inafanyika kulingana na vile mtafiti alivyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti. Utafiti huu ulifanyika nchini Kenya ambapo mtafiti alitembelea jimbo la Siaya haswa mji mkuu wa jimbo hili ambao ni Siaya kuliko na majengo makuu ya bunge kunakokutana wajumbe kufanyia mijadala.

Utafiti huu ulijikita kwenye matumizi ya lugha katika shughuli za kisiasa na kuchunguza nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha ya mijadala ya wajumbe bungeni katika kaunti ya Siaya.

Vilevile, mtafiti alitembelea maktaba za vyuo vikuu vya Maseno, Jaramogi Oginga Odinga na Mount Kenya kwani kulipatikana majarida, tasnifu pamoja na maandishi maridhawa yaliyohusiana na mielekeo ya uteuzi wa lugha kwenye miktadha mbalimbali.

3.3 Walengwa wa Utafiti

Kundi lengwa ina maana ya wanachama, kundi, mtu, watu au elementi zinazokusudiwa kuhusishwa na mtafiti katika kazi. Haya ni kwa mujibu wa Looper mwaka wa (1989) na Varis mwaka wa (1990). Kulingana na Kothari mwaka wa (2004), Bryman mwaka wa (2004), Kombo na Trump mwaka wa (2006), kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika mchakato mzima wa utafiti. Katika utafiti huu, walengwa walikuwa wajumbe wa bunge la Siaya waliochaguliwa kuwakilisha wodi mbalimbali kwenye bunge la kaunti hiyo.

Jedwali 1: Idadi ya Wawakilishi Wodi wa Jimbo la Siaya

| Eneo Bunge | Wodi | Idadi ya Wawajumbe |
|---------------------|------------------|--------------------|
| Alego Usonga | North Alego | 6 |
| | West Alego | |
| | Central Alego | |
| | Siaya Township | |
| | South East Alego | |
| | Usonga | |
| Bondo | West Yimbo | 6 |
| | Central Sakwa | |
| | South Sakwa | |
| | Yimbo East | |
| | West Sakwa | |
| | North Sakwa | |
| Gem | North Gem | 6 |
| | West Gem | |
| | Central Gem | |
| | Yala | |
| | Township | |
| | East Gem | |
| Ugenya | South Gem | 4 |
| | West Ugenya | |
| | Ukwala | |
| | North Ugenya | |
| | East Ugenya | |

| | | |
|------------------------|--|----|
| Rarieda | East Asembo | 5 |
| | West Asembo | |
| | North Uyoma | |
| | South Uyoma | |
| | West Uyoma | |
| Ugunja | Sidindi | 3 |
| | Sigomere | |
| | Ugunja | |
| Wajumbe Maalum | Wawakilishi wa makundi maalum kwa mfano vijana, wachache na walemavu | 12 |
| JUMLA | | 42 |
| Asili: Kaunti ya Siaya | | |

3.4 Sampuli na Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Babble mwaka wa (1992), sampuli ina maana ya sehemu inayovutia mtafiti kwa nia ya kupata taarifa fulani kwa lengo la kutoa hitimisho la utafiti anaokusudia kutekeleza. Sampuli huwa ni kitu kimoja kinachopatikana kati ya vitu vingi vya aina moja na ambacho huchukuliwa kama mfano mwema wa kuwakilisha vitu vingine vilivyobaki, TUKI mwaka wa (2012). Vilevile, Kothari mwaka wa (2009), anaeleza ya kwamba sampuli ni kundi dogo la wanaotafitiwa na ambalo huteuliwa na mtafiti ili litumike kuwakilisha kundi kubwa lililobaki na ambalo kwalo mtafiti hupata data anayonua kutumia kutoa hitimisho la utafiti wake. Kulingana na Kothari mwaka wa (1990), sampuli iliyoteuliwa hupaswa kuwa na kipimo fulani kisicho na watu wachache sana au wengi na ambayo sharti iweze kutosheleza mahitaji aliyokusudia.

Hivyo basi jimbo la Siaya linapatikana katika ukanda wa magharibi mwa Kenya hususani uliokuwa mkoa wa Nyanza viungani mwa Ziwa Viktoria. Kulingana na katiba mpya ya Kenya mwaka wa (2010) iliyoorodhesha majimbo kulingana na nambari, jimbo la Siaya limepewa nambari arobaini na moja (41). Kwa kutumia sampuli ya matilaba, bunge la jimbo hili ndilo lilituuliwa kuwa eneo la utafiti. Bunge hili ndilo liliwakilisha mabunge arobaini na saba na

kuchunguza haswa yanayochochea uteuzi wa mielekeo ya lugha wakati wa mijadala. Wengi wa wenyeji wa kaunti ya Siaya ni Waluo walio na lafudhi tofauti za mazungumzo.

Wajumbe wote wa jimbo la Siaya ni arobaini na wawili (42). Utafiti huu ulitumia mbinu ya kimaksudi kuchagua wajumbe thelathini (30) walioteuliwa moja kwa moja na wapiga kura kuwakilisha wodi katika jimbo hili la Siaya. Hii ni asilimia sabini na moja nukta nne tatu (71.43%) ya jamii lengwa. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji elekezi, mtafiti aliteua wawakilishi wa wananchi bungeni humu ili kupata data ya anachotaka kufanyia utafiti wake. Vile vile, mtafiti alitembelea wananchi kwenye vikao rasmi na visivyo rasmi kwa nia ya kupanua wingi wa data yake kuhusu uteuzi wa lugha inayodhibiti mielekeo ya matumizi kwa wajumbe wao. Kwa jumla, miktadha teule ilikuwa ya manufaa makubwa katika kuyatimiza malengo ya utafiti huu na hata kuibuka na data kwa wingi ili kufanikisha utafiti huu.

3.5 Mbinu na Vifaa vya Kukusanya Data

Mbinu ni njia ya kutekeleza jambo fulani TUKI mwaka wa (2012). Utafiti huu utahusisha mbinu mbili kuu za uchunguzi; ile ya maktabani na ya nyanjani. Mbinu hizi zitatumika ili kumwezesha mtafiti kupata data inayohitajika ikiwemo ya msingi na upili. Katika mchakato mzima wa utafiti, mtafiti alitumia kalamu na karatasi za kuandika kumbukumbu, tepurekoda ilitumika kurekodi sauti za watafitiwa, tarakilishi ilitumika kuhifadhi data iliyokusanywa, pia simu ilitumika kutafiti katika mtandao wa intaneti. Mwishowe, karatasi za hojaji zenye maswali tofauti yanayolenga swali la utafiti zilitumika.

3.5.1 Utafiti wa Maktaba

Kazi za uandishi wa aina tofauti hupatikana kwenye maktaba zikiwemo vitabu, majarida, ripoti za watumishi wa umma pamoja na hifadhi nyingi zilizosheheni maarifa ya kuauni mtafiti yeyote yule. Upitiaji wa kazi hizi za waandishi waliobobea na chipukizi ulimwezesha mtafiti kuimarisha

viwango vyake vya uelewaji wa mada ya utafiti na kisha ukamwezesha kuwa na ujuzi pindi alipofunga safari ya kwenda nyanjani kuishughulikia kazi ya utafiti wake.

Vile vile, kule maktabani mtafiti alipata nafasi bora ya kusoma maandishi yanayohusiana na lugha za jamii za magharibi mwa Kenya na haswa ukanda wa Ziwa Viktoria kabla na baada ya uhuru na kuelewa zaidi kuhusu historia za jamii hizi kwa mapana. Kule maktabani pia yalisomwa yale yote yanayohusiana na nadharia ambapo mtafiti alipata mwongozo mwafaka wa kitaaluma alipokuwa akifanya utafiti wake. Aidha, maandishi yaliyopitiwa na mtafiti yalimwanzia kufikia mbinu za kukusanya data pamoja na kuichanganua na kuyawasilisha matokeo ya utafiti husika.

3.5.2 Utafiti wa Nyanjani

Utafiti wa nyanjani ulifanywa kwa lengo la kufidia upungufu wa yaliyoandikwa kuhusu nafasi ya mielekeo katika uteuzi wa lugha. Sampuli ya matilaba ilitumika kule nyanjani ili kumwongoza mtafiti kutembelea maeneo tofauti katika jimbo la Siaya haswa majengo ya bunge ili kuhoji wajumbe waliochanguliwa kwenye wodi mbalimbali kuwakilosha wananchi bungeni na kurekodi mazungumzo kwenye mikutani rasmi na isiyo rasmi.

Miktadha halisi ya matukio tofauti yalizingatiwa wakati wa kukusanya data. Ili kurutubisha data, mtafiti aliteua mikusanyiko ya wajumbe na kuwa na vikao nao kwa sababu hao ndio waathiriwa wakubwa katika uteuzi wa mielekeo ya lugha wakati wa mijadala.

3.6 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Matokeo ya Data itakayokusanywa

Kwa mujibu wa Coursera mwaka wa (2022), uchambuzi wa matokeo ya data ni mazoezi ya kufanya kazi na data iliyokusanywa na kukusanya taarifa muhimu ambayo inaweza kutumika kufanya maamuzi sahihi. Ni mchakato wa kutumia kwa utaratibu mbinu za takwimu na au za

kimantiki kueleza na kuonyesha, kufupisha na kudhamini data iliyokusanywa.

Zipo mbinu tofauti za uchambuzi wa matokeo ya data zikiwemo zile za maelezo, maagizo na utambuzi. Hata hivyo, data zilizokusanywa na utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo na tarakimu kwani mbinu hizi humpa mtafiti ruhusa ya kusikiliza au kusoma kisha kuelewa vyema maudhui aliyonua kuangazia.

Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kunukuu na kunakili katika karatasi na kisha kuchambuliwa kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti. Utafiti wenyewe uliongozwa na nadharia za Vitendo Vilivyofiriwa iliyoasisiwa na Fishbein pamoja na Nadharia Jumuishi ya Utambulisho iliyoasisiwa na Giles.

3.7 Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Mathooko na wenzie mwaka wa (2007), maadili ya utafiti ni ule uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote wanaotangamana na mtafiti katika mchakato mzima wa utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Barnes mwaka wa (2000) anasema maadili huibuka wakati mtafiti anapojaribu kuamua kati ya chanzo cha tendo kwa tendo lingine sio kwa manufaa tu lakini kwa kurejelea mienendo mizuri au mibaya.

Kulingana na Massamba (2009), maadili ya utafiti sio suala la kidhahania kwani hutokea katika eneo mahususi na kwa watu mahususi. Vipengele vinavyohusiana na maadili ni pamoja na kuomba na kukabidhiwa kibali cha kufanya utafiti wa kutunza siri zote za taarifa, ridhaa za watakaotafitiwa pamoja na uchukuaji wa picha zao na za mazingira yao. Hii ina maana kuwa mtafiti yeyote yule hawezi kuliepuka suala nyeti la maadili.

Kabla ya kuzamia utafiti wake, mtafiti aliomba kukabidhiwa stakabadhi muhimu kama vile; cheti

cha kuanzisha utafiti wake kutoka Chuo kikuu anachosomea mtafiti cha Mount Kenya, kile cha kufanya utafiti kutoka kwa kitengo cha idhini za ukusanyaji wa data nchini NACOSTI. Vilevile, mtafiti alipata vyeti vya kumruhusu kufanya utafiti kutoka kwa uongozi wa jimbo la Siaya ukiwemo ule wa majengo ya mabunge hili. Utafiti huu ulifanywa kwa uwazi na uadilifu mkubwa huku nyadhifa zote husika zikitambuliwa na kuheshimiwa. Data iliyozalishwa ni ya ukweli na ya kuaminika na ambayo pia itakuwa na nafasi ya kudhibitishwa na watafiti baadaye.

3.8 Hitimisho

Sura hii ya tatu imeshughulikia vipengele vya mbinu za utafiti ambavyo vilijadiliwa. Vipengee hivyo ni pamoja na; ule Muundo wa utafiti, Mahali ambapo utafiti ulifanyika, Walengwa wa utafiti, Sampuli pamoja na uteuzi wake, Mbinu na Vifaa vilivyotumika kwenye mchakato wa kukusanya data na kisha mbinu zilizotumika kukusanya data; ile ya maktabani na ya nyanjani na hatimaye uchambuzi, uwasilishaji wa data na maadili yaliyoongoza utafiti.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA DATA, UFAIRI NA MATOKEO YA UTAFITI

4.0 Utangulizi

Katika sura hii ya nne, ujumbe mfupi kuhusu jimbo la Siaya utaangaziwa japo kwa muhtasari. Vile vile, kauli za mielekeo ya wajumbe kuhusu uteuzi wa lugha ziliangaziwa kwa undani wake. Sababu za wajumbe kuwa na mtazamo fulani zilichanganuliwa kwa lengo la kusoma akili za wajumbe wa kaunti ya teule. Vielelezo pamoja na majedwali kuhusiana na vipengele vya kauli za sababu za mielekeo ya wajumbe zimechorwa katika sura hii.

4.1 Muktaba wa Kiisimu wa Eneo la Utafiti

Kaunti ya Siaya ambayo ni mojawapo ya kaunti arobaini na saba 47 nchini Kenya, hupatikana katika ukanda wa Magharibi mwa Kenya eneo la ziwani Viktoria. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya (2010), Kaunti hii ni nambari arobaini na mbili (42). Kaunti hii hupakana na Kaunti ya Busia upande wa Kaskazini, Kaunti za Kakamega na Vihiga upande wa Kaskazini Mashariki, na Kaunti ya Kisumu upande wa Kusini Mashariki. Kaunti hii pia imegawanywa na Kaunti ya Homa Bay na Ziwa Victoria upande wa Kusini. Ukubwa wa Kaunti ya Siaya ni kilomita 2,496 mraba. Kaunti hii pia imegawanywa kwa kaunti ndogo saba zikiwemo: Alego Usonga, Bondo, Gem Yala, Gem Wagai, Rarienda, Ugenya na Ugunja. Makao makuu ya Kaunti hii yako mjini Siaya. Kaunti hii ina idadi ya wakaazi 993,183 kwa mujibu wa takwimu za idadi ya Wakenya (KNBS, 2019). Lugha zinazozungumzwa katika Kaunti hii ni Dholuo, Kiswahili, Kiingereza na zile za makabila yanayopakana na kaunti ya Siaya.

4.1 Uchanganuzi wa Data Kuhusu Mielekeo ya Lugha ya Wajumbe

Lengo la kwanza ambalo ni kuchunguza iwapo mielekeo inachangia uteuzi wa lugha inayotumika katika mijadala bungeni, lengo la pili ambalo ni kuchambua iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya wana

sababu maalumu zinazowapelekea kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine katika mijadala yao bungeni, lengo la tatu ambalo ni kuchunguza iwapo kuna lugha mahususi inayopendelewa na wajumbe katika mijadala yao bungeni pamoja na lengo la nne ambalo ni kuchunguza iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia wajumbe wa kaunti ya Siaya kutumia Kiswahili kufanikisha mawasiliano katika muktadha wa mijadala bungeni yamechanganuliwa kwa undani wake. Katika utafiti uliofanywa, wajumbe waliochaguliwa na wapiga kura kuwakilisha wodi mbalimbali katika kaunti ya Siaya ndicho kigezo kilichotumika ili kusaidia katika uchanganuzi wa data ili kutathmini mielekeo yao ya lugha katika mijadala bungeni. Kigezo cha wajumbe waliochaguliwa kilizingatiwa katika utafiti huu kwa vile wajumbe walioteuliwa na vyama, makarani pamoja na waelekezi wa mijadala katika bunge la Siaya walionekana kuwa na mielekeo tofauti kuhusu uteuzi wa lugha ya mijadala katika bunge hili linalotumika kuunda sheria zinazoongoza serikali na wakaazi wa kaunti ya Siaya. Utafiti huu ulifanywa miongoni mwa wajumbe waliochaguliwa kwa kupigiwa kura na wananchi wa kaunti hii ili kuwakilisha maslahi yao bungeni.

Mihimili ya Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa iliyoasisiwa na Ajzen na Fishbein (1980) inaeleza kuwa ili kuelewa vyema tabia au mielekeo ya watu kuhusu jambo linalotakikana kushughulikiwa, ni lazima kisababishi cha tabia ile kitathminiwe kwa kupitishwa kwenye vipimo vya mbinu mbalimbali kama vile mahojiano, uchunzaji au hojaji. Kwa vile mielekeo ya binadamu huweza kudhihirika wazi kwa matendo yake au ikajificha kwenye akili yake, hubidi mtafiti aliye na nia ya kuchunguza mielekeo husika kutumia mbinu lengwa mbalimbali ili kubaini ukweli wa kauli anazotaka kutafitia.

Hivyo basi, mtafiti anaweza kuamua kutumia mbinu ya uchunzaji ili kupima mielekeo inayodhihirika wazi. Vile vile, ili kupima mielekeo inayodhihirika kwenye akili ya binadamu huyu, mtafiti anaweza kutumia mbinu ya mahojiano au hata hojaji. Katika utafiti huu, data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji zilizo na kauli tano ambazo zilikabidhiwa wajumbe waliochaguliwa ili wajaze ambapo

kutokana na waliojaza, mielekeo yao kuhusu uteuzi wa lugha ya mijadala bungeni ilidhihirika. Hojaji ambayo ilikuwa na kauli ishirini iliweza kutumiwa kupima akili za wajumbe kuhusu mielekeo ya uteuzi wa lugha ya mijadala. Katika kila kauli, kulikuwa na majibu matano ambapo wajumbe walihitajika kuchagua jibu moja ambalo liliachilia iwapo walikuwa na mwelekeo chanya au hasi kuhusu kauli husika ya lugha. Majibu hayo matano yalikuwa ni pamoja na;

- i) Nakubali kikamilifu
- ii) Nakubali
- iii) Sina uhakika
- iv) Nakataa
- v) Nakataa kikamilifu

Katika mchakato wa kujaribu kukusanya taarifa kuhusu mielekeo ya wajumbe kuhusu uteuzi wa lugha ya mijadala bungeni katika kaunti ya siaya, utafiti huu ulihusisha wajumbe wote walioteuliwa na wapiga kura ili kuwawakilisha kwenye wodi zao ambao ni wajumbe thelathini (30). Wahojiwa ishirini na saba (27) ambao ni asilimia tisini (90%) ya jumla ya wajumbe waliweza kujaza na kurudisha hojaji zao zikisheheni wingi wa data iliyohitajika na mtafiti. Kiwango hiki cha juu kiliafikiwa kutokana na juhudi za mtafiti kusambaza hojaji yeye binafsi na kuchukua muda wake vyema kwa kusubiri wahojiwa wake kukamilisha kazi yao bila bughudha. Asilimia kumi (10%) ya wajumbe ambao ni watatu (3) haikuweza kurejesha hojaji zao kutokana na sababu zao za kibinafsi ambazo mtafiti hakuzielewa kwani walitumia ujanja wao na kuhepa na karatasi za hojaji. (Taz. jedwali 1).

Jedwali 2: Kiwango cha Mwitikio

| | Idadi ya Mwitikio | Asilimia (%) |
|-----------------------------------|--------------------------|---------------------|
| Hojaji zilizojihiwa | 27 | 90 |
| Hojaji ambazo hazikujibiwa | 3 | 10 |
| Jumla | 30 | 100 |


Asili: Mtafiti

Kwa jumla, kulingana na majibu matano yaliyotolewa kwa wajumbe, jibu la kwanza na la pili liliashiria mwelekeo chanya, yaani wajumbe wa kaunti ya Siaya walikuwa na mtazamo kubalifu kuhusu uteuzi wa lugha ya mijadala bungeni. Jibu la tatu lilionyesha kuwa wajumbe hawakuwa na mwelekeo wowote ilhali jibu la nne na la tano lilionyesha mwelekeo hasi, yaani wajumbe hawakuwa na mtazamo kubalifu kuhusu uteuzi wa lugha ya aina fulani inayohitajika kutumiwa wakati wa mijadala bungeni. Majibu yaliyokokotwa kutoka kwa hojaji yaliweza kuchanganuliwa kupitia mtindo wa tarakimu sayansi na yakawekwa kama ifuatayo:

4.1.1 Urahisi wa Kujifunza Kiswahili

Kulingana na kauli hii, wajumbe kumi na watano (15) yaani asilimia hamsini na tano nukta tano sita (55.56%) walikubali kikamilifu kuwa ni rahisi kujifunza lugha ya Kiswahili kwani ni lugha ya kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Kenya mwaka wa (2010) na hivyo basi ni lugha ya kuwaunganisha wananchi. Wajumbe waliosalia walikuwa na mtazamo wa asilimia sawa kwani watatu(3); asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) walikubali kiasi kuwa ni rahisi kujifunza Kiswahili, wajumbe wengine watatu (3); asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) hawakuwa na uhakika kuhusiana na kauli hii huku idadi ya wajumbe wengine watatu(3); asilimia hiyo hiyo kumi na moja nukta moja moja (11.11%) wakikataa madai kuwa ni rahisi kujifunza lugha hii ya kitaifa ilhali idadi hiyo hiyo ya wajumbe watatu(3) yaani asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%)

wakikataa kabisa kwa kudai kuwa ni vigumu kujifunza lugha ya Kiswahili licha ya kuwa ni lugha ya kitaifa kulingana na katiba ya nchi.(Taz. kielelezo 1).




Kielelezo 1: Urahisi wa Kujifunza Kiswahili

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha waziwazi kuwa asilimia kubwa ya wajumbe waliochaguliwa katika Kaunti ya Siaya wanaonelea kuwa hakuna ugumu wowote wa kujifunza Lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wengi wao wamepitia masomo ya msingi, sekondari na wengine vyo vikuu ambapo mara nyingi lugha hii ilikuwa somo la lazima na la kutahiniwa kwenye mitihani ya shule na ile ya kitaifa. Asilimia kubwa ya waliokubaliana na kauli hii ni ishara tosha kuwa wajumbe wengi wana mielekeo chanya kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa vile wajumbe wana sababu maalum ya urahisi wa ujifunzaji wa Kiswahili.

4.1.2 Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya kutoa Hoja katika Mijadala Bungeni

Mtafiti alinua kupata taarifa ya kubaini ikiwa wajumbe kwenye Kaunti hii ya Siaya wanapenda

kutumia lugha ya Kiswahili kutoa hoja zao katika mijadala yao bungeni. Kutokana na kauli hii, ilidhihirika kuwa asilimia kubwa ya wajumbe ambayo ni wajumbe ishirini (20) yaani asilimia sabini na nne nukta sufuri saba (74.07%) walipenda zaidi kutumia Kiswahili wakati wanapotoa hoja zao kwenye bunge. Wajumbe wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) walikubali kauli hii kwa wastani tu huku wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikosa uhakika, wawili (2) wengine yaani asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikataa kauli hii na mwingine mmoja (1); ambayo ni asilimia tatu nukta saba (3.70%) kupinga kauli hii kwa dhati. (Taz. Kielelezo 2)




Kielelezo 2: Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Kutoa Hoja Bungeni

Kulingana na matokeo ya kauli hii ni dhahiri kuwa wajumbe wengi wanakienzi Kiswahili kama lugha inayoeleweka kwa urahisi na hivyo basi wanapendelea kukitumia wakati wa mijadala ili kuufikisha ujumbe wao vyema kwa waliohudhuria vikao vya bunge. Hili linabainisha waziwazi kuwa wajumbe wengi wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kwani wanapenda kutumia Kiswahili katika utoaji wa mijadala yao bungeni. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa

vile wajumbe wa jimbo la Siaya wanapendelea lugha ya Kiswahili katika mijadala yao bungeni.

4.1.3 Uelewaji wa Ujumbe unaowasilishwa katika Lugha ya Kiswahili

Kwa vile kiini kikuu cha kufanya mijadala bungeni ni kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji, utafiti huu ulilenga kubaini dhana kuwa ujumbe uliowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili hufikia wajumbe vyema zaidi kuliko wakati ambapo ujumbe huu umewasilishwa na lugha nyingine na haswa Kiingereza. Kwa mujibu wa kauli hii, wajumbe ishirini na watatu (23) yaani asilimia themanini na nane nukta mbili (85.20%) walikubali kikamilifu, huku wajumbe waliosalia wakiingia mmoja mmoja kwa majibu yaliyosalia. Yaani mjumbe mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) alikubali kwa wastani naye mjumbe mwingine mmoja (1) asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikosa uhakika. Vile vile mjumbe mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) alikataa huku mwingine mmoja (1); asilimia hiyo hiyo tatu nukta saba (3.70%) pia akikataa kikamilifu. (Taz. kielelezo 3)




Kielelezo 3: Uelewaji wa Ujumbe unaowasilishwa katika Kiswahili

Kulingana na kauli hii ni kweli kuwa wajumbe wengi kwenye bunge la kaunti ya Siaya walihisi salama kutumia lugha hii ya Kiswahili wakati wa mijadala yao kwa vile hisia za wajumbe wenzao zilionyesha kuelewa ujumbe vyema. Kutokana na majibu ya wajumbe kuhusiana na kauli hii ni kuwa wengi wao wana mielekeo chanya ya kutambua kuwa wajumbe wenzao wanaelewa ujumbe unaosemwa kwa Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa vile matarajio ya uelewekaji wa ujumbe inachangia uteuzi wa lugha ya Kiswahili.

4.1.4 Dhima Kiswahili katika Maendeleo ya Taifa la Kenya

Katiba ya Kenya (2010) inaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya kuunganisha Wakenya kwa minajili ya kuendesha taifa hili kiuchumi. Hivyo basi, mtafiti alitaka kusaka mchango wa lugha hii katika dhima yake kwa maendeleo ya taifa la Kenya kutoka kwa wajumbe wa kaunti ya Siaya. Hojaji zilizojazwa na kurudishwa na wajumbe zilithibitisha kauli hii kwa viwango tofauti. Wajumbe kumi na mmoja (11) yaani asilimia arubaini nukta saba nne (40.74%) walikubali kikamilifu, wajumbe wane (4); asilimia kumi na nne nukta nane mbili (14.82%) wakakubali kwa kiwango cha wastani, mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akakosa uhakika huku watano (5) yaani asilimia kumi na nane nukta tano mbili (18.52%) wakikataa nao wajumbe sita (6); asilimia ishirini na mbili nukta mbili mbili (22.22%) wakikataa kikamilifu.




Kielelezo 4: Dhima ya Kiswahili katika Maendeleo ya Taifa la Kenya

Kwa mujibu wa kauli hii ilidhihirika kuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa Siaya walikuwa na mtazamo chanya kuwa lugha ya Kiswahili ina dhima kubwa kwa kupiga jeki maendeleo ya taifa la Kenya huku kukiwa na idadi ya wastani iliyopinga kauli hii. Wajumbe wengi wanaonekana wakiwa na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwa kuwa walikubaliana na kauli kuwa Kiswahili ni kiungo kikuu cha maendeleo ya taifa. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani dhima ya Kiswahili katika maendeleo ya taifa la Kenya inawasukuma wajumbe kuteua lugha ya Kiswahili dhidi ya lugha nyingine.

4.1.5 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari

Kwa vile vyombo vya habari huwa na vipindi vingi vinavyotolewa kwa lugha mbalimbali zikiwemo za mama na za kitaifa, mtafiti alinua kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya hufurahishwa na kuchangamshwa na vipindi vinavyotolewa katika lugha ya Kiswahili. Hojaji zilizojazwa na wajumbe zilitoa mitazamo tofautitofauti kama ifuatavyo; wajumbe kumi na tisa (19); asilimia sabini

nukta tatu sita (70.36%) walikubali kikamilifu, wajumbe wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakubali kwa kiwango cha wastani, wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakosa uhakika, wawili (2) wengine; asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakataa huku wawili (2) asilimia hiyo hiyo ya saba nukta nne moja (7.41%) wakikataa kwa dhati.




Kielelezo 5: Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari

Matokeo ya kauli hii yanaonyesha wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hupenda kufuatilia vipindi vinavyoendelezwa kwenye vyombo vya habari kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwani huwa vinawafurahisha na pia kuwachangamsha na kuwaburudisha. Wajumbe wengi wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani wanaonekana kufurahishwa na kuchangamshwa na vipindi vinavyotolewa katika lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari. Kauli hii inakwenda sambamba na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani wana matarajio ya kibinafsi kuhusiana na Kiswahili katika vyombo vya habari.

4.1.6 Matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika Mijadala Bungeni

Siasa ni mojawapo wa mbinu kuu za kugawana rasilmali za taifa kwani huwa za kiwango cha chini

kisichotosheleza wananchi wote. Hivyo basi, mtafiti alilenga kutumia wajumbe waliochaguliwa kwenye kaunti ya Siaya ili kusaka taarifa ya iwapo wanasiasa wengi katika kaunti hiyo walipendelea kutumia lugha ya Kiingereza katika mijadala bungeni. Matokeo ya hojaji yaliashiria yafuatayo; wajumbe watatu (3) yaani asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) walikubali kikamilifu ukweli wa kuwa wanasiasa wengi hupendelea kutumia lugha ya kiingereza katika mijadala bungeni, wengine wawili (2) asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakubali katika kiwango cha wastani, mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) alikuwa na shauku kuhusu kauli hii huku wajumbe kumi (10) yaani asilimia thelathini na saba nukta sufuri nne (37.04%) wakikataa nao wajumbe kumi na mmoja(11); asilimia arubaini nukta saba nne (40.74%) wakikataa kauli hii ya matumizi ya Kiingereza katika mijadala ya bungeni.




Kielelezo 6: Matumizi ya Kiingereza katika Mijadala Bungeni

Kauli hii ilionekana ikitoa matokeo ya kuwa wajumbe wengi kwenye kaunti ya Siaya walikuwa na mtazamo hasi kuhusu matumizi ya Kiingereza katika mijadala ya bungeni huku wachache tu

wakikubaliana na kauli hii. Hii ni ishara tosha kuwa wengi wao wana mielekeo hasi kuhusu kauli hii kwani hawapendi kutumia Kiingereza wakati wa mijadala yao bungeni, hivyo wana mielekeo Chanya kuhusu matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika mijadala ya bungeni. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumuishwa wa Utambulisho kwa vile yaonekana kuna vikwazo vinavyotinga matumizi ya Kiswahili kufanikisha mawasiliano.

4.1.7 Ugumu wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha katika Mijadala Bungeni

Kwa vile lugha ya Kiswahili ni somo linalotahiniwa shule za msingi na sekondari kama la lazima, mtafiti alikuwa na shauku ya kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya hupatana na ugumu wowote wa kuongea lugha hii haswa hadharani. Pia alitaka kuchunguza kiwango cha mazoezi kinachohitajika iwapo kungekuwa na ugumu wa kuongea lugha hii ya taifa. Matokeo kwenye hojaji zilizojanjwa na wajumbe yalionyesha kuwa wajumbe wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) walikubali kikamilifu kuwa walikuwa na ugumu wa kuongea lugha hii licha ya kufanya mazoezi ya haja, wajumbe wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) walikubali kwa kiwango cha wastani, mjumbe mmoja (1) yaani asilimia tatu nukta saba (3.70%) hakuwa na uhakika wa swali hili huku wajumbe kumi (10); asilimia thelathini na saba nukta sufuri saba (37.04%) wakikataa nao wengine kumi na wawili (12) yaan asilimia arobaini na nne nukta nne nne (44.44%) wakikataa kikamilifu.




Kielelezo 7: Ugumu wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha Bungeni

Kulingana na matokeo ya kauli hii, ni wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya wanapenda Kiswahili na hawana ugumu mwingi kukiongea. Hivyo basi hawahitaji mazoezi mengi ili kumakinika na lugha hii ya Kiswahili. Matokeo ya kauli hii yanadhihirisha kuwa wajumbe wengi wana mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwani hawapati ugumu wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa kwa sababu maalumu ya kuteua Kiswahili ni kule kukosa ugumu wa kuizungumza lugha hii ya taifa.

4.1.8 Athari za Makosa ya Kimatamshi katika Matumizi ya Kiswahili

Mtafiti alikuwa na moyo wa kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya huwa na matamshi tata ya maneno ya Kiswahili na iwapo kuna wanaowacheka wanapotatizika kimatamshi. Wajumbe waliojaza na kurudisha hojaji zao walitoa ujumbe ufuatao. Mjumbe mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) alikubali kikamilifu kuwa hapendi kutumia Kiswahili kwa vile utata wa matamshi yake hufanya wajumbe wenzake wamcheke. Mjumbe mwingine mmoja (1); asilimia tatu nukta saba

(3.70%) alikuwa na ukubalifu wa wastani kuhusiana na kauli hii, mmoja (1) asilimia hiyo hiyo tatu nukta saba (3.70%) pia akawa na jibu la kukosa uhakika huku wajumbe kumi na saba (17); asilimia sitini na mbili nukta tisa saba (62.97%) wakikataa na wengine huku wajumbe saba (7); asilimia ishirini na tano nukta tisa tatu (25.93%) wakikataa kauli hii kwa kuonyesha ukakamavu wao wa kuongea Kiswahili bila hofu yoyote.




Kielelezo 8: Athari za Makosa ya Kimatamshi katika Matumizi ya Kiswahili

Matokeo ya kauli hii yalionyesha peupe kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya wanajiamini na hawana woga kuongea Kiswahili kwani wana matamshi bora ya maneno ya lugha hii. Hii ni ishara tosha kuwa wanakienzi Kiswahili tangia masomo yao ya shuleni baada ya kutambua kuwa ni somo la lazima. Hivyo basi, wengi wao wanaonekana kuwa na mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwa kuwa hawaogopi kuchekwa na wenzao wanapotamka kwa Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwani wajumbe husika hawana vikwazo vinavyotinga matumizi ya Kiswahili kwani matamshi yao yako sawa.

4.1.9 Kuchanganya Lugha wakati wa Kutoa Hoja Bungeni

Kwa vile nia kuu ya kuzungumza ni kufikisha ujumbe kwa msikilizaji, mtafiti alikuwa na haja ya kutaka kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya huwa wanatumia mtindo wa kuchanganya lugha wanapotoa hoja zao katika mijadala bungeni kwa lengo la kueleweka vyema. Wajumbe wengi walikubaliana na kauli hii kwani matokeo ya hojaji yalikuwa yafuatayo: wajumbe kumi na wane (14); asilimia hamsini na mmoja nukta nane tano (51.85%) walikubaliana na kauli hii kwa ukamilifu, wajumbe sita (6); asilimia ishirini na mbili nukta mbili mbili (22.22%) wakakubali kwa kiwango cha wastani, wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakosa uhakika wa kauli hii huku wajumbe wengine watatu (3); asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) wakikataa na wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) kupinga kauli hii kwa dhati. (Taz. kielelezo 9)




Kielelezo 9: Kuchanganya Lugha wakati wa Kutoa Hoja Bungeni

Kulingana na matokeo ya kauli hii ni wazi kuwa mara nyingi wajumbe wa kaunti ya Siaya hupendelea kuchanganya lugha wanapotoa mijadala yao bungeni kwani kuna maneno yaliyo na ugumu kueleweka kwa Kiswahili. Hii ni ishara tosha kuwa wengi wao wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii ya kuchanganya lugha ili kueleweka vyema na wenzao. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani matarajio ya kibinafsi ya kutaka wajumbe wenzao wawaelewe vyema huwalazimu kuteua Kiswahili wakati wa mjadala bungeni.

4.1.10 Utoaji Hotuba kwa Wananchi kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili

Wanasiasa huhitaji kutangamana na wananchi moja kwa moja kwani ni kwa hisani zao wanapata nafasi ya kujiunga na bunge. Hivyo basi wanasiasa hawa hawana budi kuhakikisha kuwa wanazungumza na wapiga kura kwa lugha wanayoielewa zaidi ili kuwa na ufahamu wa matakwa yao. Hivyo basi, mtafiti alitaka kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya hupenda kutumia Kiswahili kilicho lugha ya taifa wanapowasiliana na wananchi wanaowakilisha bungeni. Hojaji zilitoa matokeo yafuatayo kuhusiana na kauli hii. Wajumbe kumi na sita (16); asilimia hamsini na tisa nukta mbili saba (59.27%) walikubaliana kikamilifu na kauli hii. Wengine watatu (3); asilimia kumi (11.11%) walikuwa na ukubalifu wa wastani huku mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikosa uhakika wa kauli hii, wajumbe watatu (3); asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) wakikataa nao wanne (4); asilimia kumi na nne nukta nane moja (14.81%) pia wakipinga kauli hii kwa ukamilifu wao. (Taz. kielelezo 10)




Kielelezo 10: Utoaji Hotuba kwa Wananchi kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili

Kwa mujibu wa matokeo ya kauli hii ni kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walipendelea mno kutumia lugha ya Kiswahili wanapowahutubia wanananchi wanaowakilisha ili kuelewana nao vilivyo. Hii ni ishara tosha kuwa wengi wa wajumbe wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwa vile wangependa kuwasiliana na wapiga kura wao kwa lugha wanaoelewana nayo. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani matarajio ya jamii wanamotoka wajumbe husika huwalazimu kuwa na mielekeo ya kuchangua Kiswahili katika mawasiliano.

4.1.11 Uamuzi wa Kuchangua Kutumia Kiingereza au Kiswahili

Kwa kuwa maisha ya kila siku huhitaji kuchagua baina ya vitu mbalimbali, mtafiti alikuwa na nia ya kuchunguza lugha ambayo hupendelewa na wajumbe wa kaunti ya siaya wakati kuna hitaji la kuchangua kati ya Kiingereza na Kiswahili. Baada ya wajumbe kujaza na kurudisha hojaji walizopewa, matokeo ya maamuzi yao yalijitokeza kama ifuatavyo: Wajumbe kumi na wanane (18); asilimia sitini na sita (66.68%) walikubali kikamilifu, wajumbe sita (6); asilimia ishirini na mbili

nukta mbili mbili (22.22%) wakakubali kwa wastani huku mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikosa uhakika wa kauli hii, mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikataa na mwingine mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikataa kwa ukamilifu. (Taz. kielelezo 11)




Kielelezo 11: Umuzi wa Kuchangua Kutumia Lugha ya Kiingereza au Kiswahili.

Matokeo ya kauli hii yaliashiria wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hupenda Kiswahili na iwapo wanatakiwa kufanya maamuzi ya kuchangua kati ya lugha hii na kiingereza, wao huegemea lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, wajumbe wengi wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwa vile kwao Kiswahili kina mashiko sana na hivyo endapo kuna nafasi ya kuchangua lugha ya matumizi wao hukichangua bila pigamizi. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa kwani wajumbe husika wana sababu maalumu ya kuteua lugha fulani dhidi ya nyingine.

4.1.12 Ujasiri wa Kutumia Lugha ya Kiswahili Bungeni

Kwa vile binadamu huhitaji kujivunia na kujihisi bingwa kwa anachopenda kukifanya maishani, mtafiti alikuwa na shauku ya kuchunguza iwapo wajumbe waliochaguliwa kuwakilisha wananchi bungeni katika kaunti ya Siaya hujivunia wanapotumia lugha ya Kiswahili bungeni. Wajumbe hao walikuwa na mitazamo tofauti kama ilivyodhihirika kwenye hojaji zao kama ifuatavyo: Wajumbe ishirini (20) yaani asilimia sabini na nne nukta sufuri saba (74.07%) walijihisi mashujaa kikamilifu wa kusema kuwa lugha ya Kiswahili wakati wanapotoa mijadala bungeni, wajumbe wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakubali kwa wastani, mbunge mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akakosa uhakika wa kauli hii, huku wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakataa na wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) pia wakakataa kwa ukamilifu kabisa. (Taz. kielelezo 12)




Kielelezo 12: Ujasiri wa kutumia Lugha ya Kiswahili Bungeni

Matokeo ya kauli hii yalikaariri ukweli kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hujihisi mashujaa wakubwa wanapotumia lugha ya Kiswahili bungeni. Ushujaa huu unatokana na mapenzi ya Kiswahili kwa mioyo ya dhati. Kauli hii inadhihirisha kuwa wengi wa wajumbe wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli husika kwani ufasaha wa lugha ya Kiswahili kwao huwafanya mashujaa wa utumizi wa misamiati yenye mnato wa kweli. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuisho wa Utambulisho kwa vile wajumbe husika hupendelea lugha ya Kiswahili ili wajihisi mashujaa.

4.1.13 Matumizi ya Kiingereza katika Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari hutumiwa kutoa mafunzo na burudani kwa wananchi wengi kupitia vipindi mbalimbali. Kwa kutilia kauli hii maanani, mtafiti alikuwa na shauku ya kujua maoni ya wajumbe wa kaunti ya Siaya kuhusu lugha inayowapendeza zaidi wakati wa kutazama vipindi kwenye televisheni. Majibu ya hojaji yalileta matokeo yafuatayo: Wajumbe wane (4); asilimia kumi na nne nukta nane mbili (14.82%) walikubaliana kabisa na kauli hii, huku wengine wane (4); asilimia kumi na nne nukta nane mbili (14.82%) wakawa na ukubalifu wa wastani, mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikosa uhakika huku watatu (3) yaani asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) wakikataa na wengine kumi na watano (15); asilimia hamsini na tano nukta tano tano (55.55%) wakikataa kabisa. (Taz. Kielelezo 13)




Kielelezo 13: Utazamaji Vipindi vya Televisheni katika Lugha ya Kiingereza

Matokeo ya kauli hii ni kuwa wajumbe wengi hawana moyo wa kutazama vipindi vya lugha ya Kiingereza kwenye televisheni kwa sababu zao za kibinafsi. Kwa kuwa na mitazamo hasi ya lugha hii ya kigeni, wajumbe hawa walikuwa na chuki na vipindi vya Kiingereza. Hii ina thibitisho kuwa wengi wa wajumbe wa jimbo la Siaya wana mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwa vile vipindi vya Kiswahili kwenye runinga huwa na mnato wake kwao na familia zao. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumishi wa Utambulisho kwa vile wajumbe wanakwazwa na lugha ya Kiingereza inayoleta vipindi katika televisheni.

4.1.14 Hisia za Unyonge wakati wa kuzungumza Kiswahili

Mtafiti alitaka kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya hujihisi wanyonge wanapoongea lugha ya Kiswahili ndani na nje ya mbunge. Wajumbe ishirini na saba waliojaza na kurudisha hojaji zao walitoa maoni mbalimbali kuhusiana na kauli hii. Wajumbe kumi na sita (16) yaani asilimia

hamsini na tisa nukta mbili saba (59.27%) walikubaliana kabisa na kauli hii, wajumbe wanne (4); asilimia kumi na nne nukta nane moja (14.81%) wakawa na ukubalifu wa wastani huku wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikosa uhakika wa kauli hii na wanne (4); asilimia kumi na nne nukta nane moja (14.81%) wakikataa na mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) kukataa kwa ukamilifu wake. (Taz. kielelezo 14)




Kielelezo 14: Hisia za Unyonge wakati wa Kuzungumza Kiswahili

Matokeo yaliyotokana na kauli hii yalidhihirisha wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hawajihisi wakiwa na unyonge wowote wanapooonea lugha ya Kiswahili ndani na nje ya bunge. Hii ni kutokana na hali kuwa hii sio lugha ya kitaifa pekee mbali pia ni lugha ya kimataifa inayoenziwa dunia nzima. Wajumbe wengi wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani hawajioni na unyonge wowote wakati wa kutumia Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa kuwa kupendelea lugha ya Kiswahili inawapa ukakamavu wa kujihisi kuwa sio wanyonge kwa vyovyote vile.

4.1.15 Ujuzi na Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili Fasaha

Umilisi wa jambo lolote huhitajika kwa yeyote aliye na ari ya kupiga hatua kubwa maishani. Huku akitilia kauli hii moyoni, mtafiti alinuia kuchunguza kiwango cha mapenzi ya kuwa na ujuzi wa umilisi wa kuzungumza Kiswahili fasaha miongoni mwa wajumbe waliochanguliwa katika kaunti ya Siaya. Baada ya wajumbe kujaza na kurudisha hojaji walizopewa, matokeo yafuatayo yalidhihirika; wajumbe kumi na wanane (18); asilimia sitini na sita (66.67%) walikubali kikamilifu, wanne (4); asilimia kumi na nne nukta nane moja (14.81%) wakakubali kwa kiwango cha katikati, mmoja (1) asilimia tatu nukta saba (3.70%) akakosa uhakika nao wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikataa na wengine wawili (2); asilimia hiyo hiyo saba nukta nne moja (7.41%) wakikataa kikamilifu. (Taz. kielelezo 15)




Kielelezo 15: Kutamani Ujuzi na Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili Fasaha

Majibu yaliyotokana na kauli hii yaliashiria wazi kuwa karibu wajumbe wote wa kaunti ya Siaya walikuwa na hamu ya kuwa na ujuzi wa umilisi wa kuzungumza Kiswahili fasaha huku wachache tu wakiwa na mtazamo hasi kuhusu kauli hii. Mielekeo chanya ya wajumbe kuhusiana na kauli hii ni kuwa wao wangependa kuwa na umilisi wa utumizi wa Kiswahili kwani ndiyo lugha ambayo hupendelewa sana na raia wanaowakilisha. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa kuwa wajumbe wengi wana matarajio ya kibinafsi ya kuwa na ujuzi na umilisi wa lugha ya Kiswahili.

4.1.16 Ufasaha wa Lugha ya Kiswahili

Ufasaha ni uwezo wa kusoma au kuzungumza kwa haraka na kwa usahihi huku ishara zikioana na uzungumzaji. Mtafiti alikuwa na nia ya kuchunguza mitazamo ya wajumbe wa kaunti ya Siaya kuhusiana na kiwango cha ufasaha wa lugha ya Kiswahili. Kulingana na hojaji za wajumbe ishirini na saba, matokeo yafuatayo yalijitokeza kwa uwazi. Wajumbe kumi na saba (17); asilimia sitini na mbili nukta tisa saba (62.97%) walikubaliana kikamilifu na kauli hii, saba (7); asilimia ishirini na tano nukta tisa tatu (25.93%) wakakubali kwa kiwango cha wastani, naye mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akakosa uhakika kuhusiana na kauli hii ya ufasaha huku mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikataa na mwingine mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) kukataa kwa dhati. (Taz. kielelezo 16)




Kielelezo 16: Kiswahili ni Lugha yenye Ufasaha kwa Wingi

Kwa mujibu wa matokeo ya hojaji za wajumbe wa Siaya ni kuwa zaidi ya asilimia themanini ya wajumbe walikuwa na mitazamo chanya kuhusiana na ufasaha ulio kwenye lugha ya Kiswahili. Ni wachache mno waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii. Mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii ni thibitisho tosha kuwa wengi wa wajumbe wanajua lugha ya Kiswahili kama iliyo na ufasaha mwingi kwani ina misamiati kwa wingi. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa kwa vile sababu moja ya kupendelea Kiswahili dhidi ya lugha nyingine ni kuwa ni lugha yenye ufasaha kwa wingi.

4.1.17 Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari

Mtafiti alinua kuchunguza iwapo wajumbe wa kaunti ya Siaya walikuwa na chuki yoyote kwa vipindi vilivyopeperushwa kwenye televisheni kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kauli hii ilitoa majibu yafuatayo kutokana na hojaji zilizojazwa na kurudishwa na wajumbe. Wajumbe kumi na wanane (18); asilimia sitini na sita nukta sita sita (66.66%) walipinga kauli hii kwa ukamilifu, wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakataa tu kwa wastani huku wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikosa uhakika na watatu (3); asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) wakiunga mkono kwa wastani na wawili (2) yaani asilimia saba nukta nne moja (7.41%) kukubaliana na kauli yenyewe kwa ukamilifu. (Taz. kielelezo 17)




Kielelezo 17: Chuki katika kusikiliza Vipindi vya Televisheni kwa Kiswahili

Matokeo ya kauli hii yalidhihirisha kuwa wajumbe wengi wa kaunti hii ya Siaya hawakukubaliana na kauli hii na hivyo basi ni ishara tosha kuwa vipindi vinanyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili ni kipenzi chao. Wajumbe wengi wana mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwani hawawezi kuchukua lugha inayoenziwa na wananchi wanaowakilisha. Hivyo, wana mielekeo Chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa kuwa wajumbe wengi hawakumbani na vikwazo wasikizapo vipindi kwa lugha ya Kiswahili.

4.1.18 Matumizi ya Kiswahili katika Ofisi na Mazingira ya Kazini

Kwa mujibu wa katiba ya Kenya mwaka wa (2010) Kiswahili ni lugha ya kitaifa inayopaswa kuzungumzwa ofisini na kwenye mazingira ya kazi kwa nia ya kuwaunganisha wahusika. Huku

akiwa na mtazamo huu kwenye akili yake, mtafiti alinua kuchunguza mitazamo ya wajumbe wa kaunti ya siaya kuhusu kauli ya iwapo lugha hii inapaswa kupigwa marufuku kwenye mazingira ya ofisini na kazini. Wajumbe walijaza hojaji na majibu yao yakadhihirisha ukweli ufuatao: Wajumbe kumi na watano (15); asilimia hamsini na tano nukta tano sita (55.56%) walipinga kauli hii kwa ukamilifu, wajumbe saba (7); asilimia ishirini na tano nukta tisa mbili (25.92%) wakapinga kwa kiwango cha wastani, wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakosa uhakika huku wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikubali kwa kiwango cha wastani na mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikubaliana na kauli hii kikamilifu. (Taz. kielelezo)




Kielelezo 18: Matumizi ya Kiswahili Yanapaswa Kupigwa Marufuku Ofisini na Kazini

Matokeo yaliyotokana na hojaji zilizojazwa kuhusiana na kauli hii yalidhihirisha wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hawakukubaliana na kauli hii. Waliashiria kuwa kuwepo kwa matumizi ya Kiswahili kwenye mazingira ya ofisini na kazini kuna manufaa makubwa kwa walioko kule. Hivyo basi wengi wa wajumbe wanaonekana kuwa na mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwani hawawezi

kubali lugha ya taifa kutupiliwa mbali katika ofisi za serikali. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumishi wa Utambulisho kwa kuwa kulingana nao hakuna vikwazo vya matumizi ya Kiswahili katika ofisi na mazingira ya kazi.

4.1.19 Matumizi ya Kiswahili Kitaifa

Kwa vile baadhi ya Wakenya na Waafrika kwa jumla huiona lugha ya Kiswahili kuwa duni kwa kuilinganisha na lugha za kigeni, mtafiti alilenga kuchunguza maoni ya wajumbe wa kaunti ya Siaya kuhusiana na kauli hii. Wajumbe wengi walionekana kupinga kauli hii kwa moyo wa dhati huku wajumbe kumi na sita (16); asilimia hamsini na tisa nukta mbili sita (59.26%) wakikataa kwa ukamilifu, sita (6); asilimia ishirini na mbili nukta mbili mbili (22.22%) wakikataa kwa kiwango cha wastani, mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akikosa uhakika huku wajumbe wawili (2) (7.41%) wakikubaliana na kauli hii na wengine wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakikubaliana nayo kikamilifu. (Taz. Kielelezo 19)




Kielelezo 19: Kiswahili ni Lugha Duni na isiyopaswa Kutumika Kitaifa

Kwa mujibu wa matokeo ya kauli hii ni dhahiri kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walionekana kupinga kauli hii kwani kulingana nao hii ni lugha kama lugha nyingine duniani na kuwa mitazamo ya Waafrika ndio walio na maoni duni mbali sio Kiswahili. Hivyo basi, wengi wa wajumbe wanaonekana na mielekeo hasi kwani Kiswahili hakiwezi kuwa duni ilhali ni lugha kimataifa. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa kuwa wao hawaoni vikwazo vya Kiswahili kuzidi kuwa lugha ya kutumika kitaifa.

4.1.20 Kiswahili ni Chombo cha Umoja wa Wakenya

Lugha ni chombo cha binadamu pekee ambacho hutumiwa kwa minajili ya kuwasiliana, kuelezana na pia kuonyesha hisia zake. Kwa vile lugha ya Kiswahili ni chombo cha kuwaunganisha Wakenya kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010), mtafiti alinuia kupata maoni ya wajumbe wa Siaya kuhusiana na kauli hii. Hojaji zilizojazwa na kurudishiwa mtafiti zilidhihirisha matokeo yafuatayo: Wajumbe kumi na watatu (13); asilimia arubaini na nane nukta moja tano (48.15%) walikubali kwa ukamilifu, wanane (8); asilimia ishirini na tisa nukta sita tatu (29.63%) wakakubali kwa kiwango cha wastani, wawili (2); asilimia saba nukta nne moja (7.41%) wakakosa uhakika huku wengine watatu (3) yaani asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) wakikataa kwa kiwango cha wastani naye mmoja (1); asilimia tatu nukta saba (3.70%) akipinga kauli hii kwa ukamilifu. (Taz. kielelezo 20)



Kielelezo 20: Kiswahili ni Chombo cha Umoja wa Wakenya

Matokeo ya hojaji ya wajumbe wa Siaya yalionyesha kuwa wajumbe wengi walikuwa na mitazamo kubalifu ya kuwa Kiswahili ni chombo cha umoja wa Wakenya kwani ni lugha iliyoenea kote nchini. Hivyo basi, wengi wa wajumbe wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani jamii ya Kenya imeshuhudia muungano ulio wazi unaoletwa na Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa vile wajumbe husika wanatarajia Kiswahili kuleta umoja wa kitaifa.

4.2 Uchanganuzi wa Sababu za Mielekeo ya Wajumbe

Katika sehemu hii sababu zilizotolewa na wajumbe kuhusiana na mielekeo yao kuhusu Kiswahili zilichanganuliwa kwa undani wake.

4.2.1 Urahisi wa Kujifunza Kiswahili

Kauli hii ilikubaliwa na asilimia sabini na saba (77%) ambao walidai kuwa baada ya Kiswahili kufanywa somo la lazima kwenye shule za msingi na upili, kuliibuka walimu waliokuwa mangwiji wa lugha hii waliojifunza kibwebwe kuifunza lugha hii na wakakumbana na urahisi wake. Vile vile, waliokubaliana na kauli hii walieleza kuwa urahisi wa kujifunza lugha hii umetokana na ongezeko la vyombo vya habari vilivyojaa vipindi vinavyopeperushwa kwa Kiswahili. Kuwa na mfuatilio wa vipindi hivi kumerahisisha ujifunzaji wa misamiati mpya inayoibuka mara kwa mara na ambayo hutumiwa na wahusika wa vipindi husika. Kwa upande mwingine, kulikuwa na asilimia 23 ya wajumbe waliokana kauli kwa kudai kuwa ndimi zao ni nzito na hivyo hushindwa kutamka vitamkwa fulani inavyotakikana.

Jedwali 3: Ni rahisi kujifunza Kiswahili

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|------|----------|----|----------|-------|----------|
| Wajumbe | 21 | 77.78 | 6 | 22.22 | 27 | 100 |

Asilimia kubwa ya waliokubaliana na kauli hii ni ishara tosha kuwa wajumbe wengi wana mielekeo chanya kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili.

4.2.2 Matumizi ya Kiswahili Kutoa Hoja katika Mijadala Bungeni

Kwa mujibu wa matokeo ya hojaji za wajumbe, asilimia kubwa ya themanini na moja nukta nne nane (81.48%) ilikubaliana na kauli hii kwa kudai kuwa kuna baadhi ya wananchi waliowachagua na ambao huhudhuria vikao vya bunge na ambao wengi wao wana kiwango cha chini cha elimu. Hivyo basi, kwao ni rahisi kuelewa Kiswahili kwani ndio lugha inayozungumzwa na watu wengi mitaani. Hata hivyo, waliopinga kauli hii na ambao ni asilimia kumi na nane nukta tano mbili (18.52%) walidai kuwa hawapendi kutoa mijadala bungeni kwa kutumia Kiswahili kwani Katiba asilia ya

Kenya imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na huwa vigumu kunukuu vipengee fulani kwa Kiswahili. Wengine waliokuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa huwa na shida za matamshi na huhofia kuchekwa na wenzao wanapokosea katika mazungumzo yao. Hii huwalazimu kutumia Kiingereza ili kuwa na mfululizo wa mazungumzo yao.

Jedwali 4: Napenda Kutumia Kiswahili Kutoa Hoja Zangu katika Mijadala Bungeni

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 22 | 81.48 | 5 | 18.52 | 27 | 100 |

Wajumbe wengi wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kwani wanapenda kutumia Kiswahili katika utoaji wa mijadala yao bungeni. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa vile wajumbe wa jimbo la Siaya wanapendelea lugha ya Kiswahili katika mijadala yao bungeni.

4.2.3 Lugha ya Kiswahili na Uelewaji Ujumbe unaowasilishwa kwa Urahisi

Wengi wa wajumbe wa kaunti ya Siaya walikuwa na mtazamo chanya kuhusu kauli kwa kiwango cha juu cha asilimia themanini na sita nukta nane tisa (86.89%) na ambao walidai kuwa ishara za wajumbe wenzao wakati wa mijadala hudhihirisha wazi kuwa huwa wanapata ujumbe vyema. Hii ilitokana na kuwa Kiswahili ndio lugha ambayo huzungumzwa na watu wengi mtaani na ambapo wajumbe wengi hutangamana na raia kwa wingi. Waliokuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii na ambao ni asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) tu walidai kuwa kuna baadhi ya wajumbe wasioelewa ujumbe vyema kwani baadhi yao walisomea ng'ambo kule ambako lugha ya Kiswahili bado haijabobea miongoni mwa taasisi za elimu.

Jedwali 5: Ninapotumia Lugha ya Kiswahili, Wajumbe Wenzangu Huelewa Ujumbe Vyema Zaidi

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 24 | 88.89 | 3 | 11.11 | 27 | 100 |

Kutokana na majibu ya wajumbe kuhusiana na kauli hii ni kuwa wengi wao wana mielekeo chanya ya kutambua kuwa wajumbe wenzao wanaelewa ujumbe unaosemwa kwa Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa vile matarajio ya uelewekaji wa ujumbe inachangia uteuzi wa lugha ya Kiswahili.

4.2.4 Dhima ya Kiswahili katika Maendeleo ya Taifa la Kenya

Wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walionekana kuwa na mtazamo chanya kuhusiana na kauli hii kwa asilimia hamsini na tano nukta tano tano (55.56 %) kwa kukubaliana na maamuzi ya katiba ya Kenya ya mwaka wa (2010). Wajumbe hawa walidai kuwa kwa vile Kiswahili ni lugha ya kuwaunganisha wakenya, basi huwaongoza kwa makubaliano ya kibiashara na pia miradi chungu nzima ya maendeleo. Walidai kuwa pasipo na lugha moja inayoongoza makubaliano ya wakenya katika sekta mbalimbali, ingekuwa vigumu kuafikia malengo ya kimaendeleo nchini. Hata hivyo kulikuwa na asilimia arubaini na nne nukta nne nne (44.44%) ambayo ilidai kuwa Kiswahili hukwaza maendeleo nchini Kenya kwani hufisha moyo wawekezaji wa mataifa ya ng'ambo wasiojua Kiswahili. Walidai kuwa mataifa mengi na haswa mashirika ya mbali kuliko na msambao duni wa Kiswahili, huhofia kuwekeza miradi yao nchini Kenya kwa kudai kuwa ni vigumu kuwa na makubaliano kwa lugha wasiyoelewa.

Jedwali 6: Lugha ya Kiswahili ina Dhima Kubwa kwa Maendeleo ya Taifa la Kenya

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|-----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 15 | 55.56 | 12 | 44.44 | 27 | 100 |

Kwa mujibu wa kauli hii ilidhihirika kuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa Siaya walikuwa na mtazamo chanya kuwa lugha ya Kiswahili ina dhima kubwa kwa kupiga jeki maendeleo ya taifa la Kenya huku kukiwa na idadi ya wastani iliyopinga kauli hii. Wajumbe wengi wanaonekana na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwa walikubaliana na kauli kuwa Kiswahili ni kiungo kikuu cha maendeleo ya taifa. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani dhima ya Kiswahili katika maendeleo ya taifa la Kenya inawasukuma wajumbe kuteua lugha ya Kiswahili dhidi ya lugha nyingine.

4.2.5 Vipindi Vinavyotolewa katika Lugha ya Kiswahili kwenye Vyombo vya Habari

Wajumbe wengi wa asilimia sabini na saba nukta saba nane (77.78%) walionekana kukubaliana na kauli hii ya kufurahishwa na kuchangamshwa na vipindi vinavyotolewa katika lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari. Kisa na maana, wao hupata ujumbe wote unaotolewa na lugha hii iliyosheheni mitaani kinyume na lafudhi za lugha za kigeni ambazo huwa na uzito wa kusikika na kueleweka vyema. Waliopinga kauli hii ambao walikuwa asilimia ishirini na mbili nukta mbili (22.22%) walidai kuwa vipindi vinavyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili havijakomaa vikilinganishwa na vinavyoundwa na kupeperushwa na wahusika kutoka mataifa ya nje. Walidai kuwa vipindi vya lugha za kigeni huwa na ubunifu wa hali ya juu na hivyo basi kuwa na mafunzo anuwai vikilinganishwa na vile vinavyoundwa Afrika Mashariki kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Jedwali 7: Kufurahia Vipindi Vinavyotolewa katika Kiswahili kwenye Vyombo vya Habari

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 21 | 77.78 | 6 | 22.22 | 27 | 100 |

Wajumbe wengi wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani wanaonekana kufurahishwa na kuchangamshwa na vipindi vinavyotolewa katika lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari.

Kauli hii inakwenda sambamba na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani wana matarajio ya kibinafsi kuhusiana na Kiswahili katika vyombo vya habari.

4.2.6 Matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika Mijadala Bungeni

Wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walionekana kupinga kauli hii kwa asilimia sabini na saba nukta saba nane (77.78%) huku wakidai kuwa kuwepo kwa wananchi wa kawaida katika vikao vya bunge huwazuia kutumia Kiingereza kwani watalemewa na kuelewa vyema. Pia walidai kuwa ukimya wa baadhi ya wajumbe wakati Kiingereza kinapotumiwa bungeni ni ishara tosha kuwa huwa hawaelewi vyema kinachosemwa. Asilimia chache ya ishirini na mbili nukta mbili mbili (22.22%) ya wajumbe waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa wajumbe wachache wanaopendelea kutumia Kiingereza kutoa hoja zao ni wale waliosomea mataifa ya nje na kutangamana na wazungu Zaidi. Hawa huhofia kutumia Kiswahili kwa kuhofia kulemewa na mazungumzo katikati ya uwasilishaji wao ambao ni kinyume na sheria za bunge zinazomhitaji mjumbe kutumia lugha moja hadi mwisho wa uwasilishaji wake.

Jedwali 8: Wanasiasa katika Kaunti Hupenda Kutumia Kiingereza katika Mijadala Bungeni

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|----------|--------------|-----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 6 | 22.22 | 21 | 77.78 | 27 | 100 |

Data katika jedwali ni ishara tosha kuwa wengi wao wana mielekeo hasi kuhusu kauli hii kwani hawapendi kutumia kiingereza wakati wa mijadala yao bungeni. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumuishwa wa Utambulisho kwa vile yaonekana kuna vikwazo vinavyotinga matumizi ya Kiswahili kufanikisha mawasiliano.

4.2.7 Ugumu wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha

Asimia chache tu ya kumi na nane nukta tano mbili (18.52%) ndiyo iliyokubaliana na kauli hii kwa kudai kuwa baada ya masomo yao ya msingi nchini Kenya, walikwenda kupanulia masomo yao ng'ambo na hivyo kusahau matamshi na misamiati fulani ya Kiswahili. Hata baada ya kurudi nchini, imekuwa vigumu kwao kujifunza lugha hii licha ya kufanya mazoezi kwa wingi. Hata hivyo asilimia ya themanini na moja nukta nne nane (81.48%) waliopinga kauli hii walidai kuwa hakuna ugumu wowote kujifunza na kuongea Kiswahili kwani ni lugha waliotangamana nayo tangu shule za msingi, upili na vyuo vikuu ambako kwa mara nyingi Kiswahili lilikuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika viwango hivyo viwili vya mwanzo yaani shule ya msingi na sekondari. Pia walieleza kuwa hii ni lugha inayozungumzwa na raia wengi mitaani wanakoishi baada ya shughuli za bunge na hivyo hurahisisha lugha yenyewe kwenye mawasiliano nao.

Jedwali 9: Ugumu wa Kuongea Kiswahili kwa Ufasaha

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|------|----------|----|----------|-------|----------|
| Wajumbe | 5 | 18.52 | 22 | 81.48 | 27 | 100 |

Matokeo ya kauli hii yanadhihirisha kuwa wajumbe wengi wana mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwani hawapati ugumu wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa kwa sababu maalumu ya kuteua Kiswahili ni kule kukosa ugumu wa kuizungumza lugha hii ya taifa.

4.2.8 Matamshi ya Kiswahili na yanavyoathiri Matumizi yake

Asilimia kubwa ya themanini na nane nukta nane tisa (88.89%) ya wajumbe wa kaunti ya Siaya walionekana kuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii. Walidai kuwa kusoma hadi vyuo vikuu na pia kutangamana na wananchi wa kawaida kila siku kumenoa matamshi yao na hivyo kuwa bora

siku baada ya siku. Hali hii huwafanya kutoa hoja zao bila wahaka wa kuchekwa na wenzao kwani hujiamini vilivyo. Asilimia ya chini ya kumi na moja nukta moja moja (11.11%) ya waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa masomo yao ya ng'ambo yaliwanyima nafasi ya kuboresha matamshi ya Kiswahili na hivyo basi hawajiamini wanapokitumia mbele ya wenzao. Pia walidai kuwa ndimi zao ni nzito kiasi cha kuunganisha silabi nzito za Kiswahili na hivyo kuhofia kuchekwa na wenzao.

Jedwali 10: Matamshi ya Kiswahili yanaathiri Matumizi yake

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|----------|--------------|-----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 3 | 11.11 | 24 | 88.89 | 27 | 100 |

Data katika jedwali inaashiria kuwa wajumbe wanakienzi Kiswahili pengine bhili linatokana na Kiswahili kuanzishwa kuwa somo la lazima katika shule za msingi na sekondari. Hivyo basi, wengi wao wanaonekana kuwa na mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwa vile hawaongopi kuchekwa na wenzao wanapotamka kwa Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwani wajumbe husika hawana vikwazo vinavyotinga matumizi ya Kiswahili kwani matamshi yao yako sawa.

4.2.9 Hali ya Kuchanganya Lugha katika Mijadala Bungeni

Wajumbe wengi walionekana kukubaliana na kauli hii kwa asilimia sabini na nne nukta sufuri saba (74.07%) kwa kudai kuwa ingawa wamebobeza kwa lugha ya Kiswahili, teknolojia inazidi kupanua mizizi yake kila uchao na hivyo kuzalisha misamiati mipya na ambayo bado haijaswahilishwa. Hili huwalazimu kuchanganya ndimi kwa kutaja misamiati husika kwa lugha yake asilia. Pia, wanapotaka ujumbe ueleweke zaidi hubidi hata watumie lugha za mama kurejelea misamiati ya vijijini iliyo na umuhimu kwa maendeleo ya kaunti yao. Wachache waliokuwa na mtazamo kinyume na kauli hii na ambao walikuwa asilimia ishirini na tano nukta tisa tatu (25.93%) walidai kuwa wao hujiaandaa vyema

kabla ya kuhudhuria vikao vya bunge na kusaka misamiati yote kwa Kiswahili na hivyo kuwafanya kutoa hoja zao kwa Kiswahili mfululizo.

Jedwali 11: Ninapotaka Wajumbe wanielewe vyema Wakati ninapotoa Hoja zangu Bungeni, mimi Hupenda Kuchanganya Lugha

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 20 | 74.07 | 7 | 25.93 | 27 | 100 |

Kulingana na matokeo ya kauli hii ni kuwa mara nyingi wajumbe wa kaunti ya Siaya hupendelea kuchanganya lugha wanapotoa mijadala yao bungeni kwani kuna maneno yaliyo na ugumu kueleweka kwa Kiswahili. Hii ni ishara tosha kuwa wengi wao wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii ya kuchanganya lugha ili kueleweka vyema na wenzao. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani matarajio ya kibinafsi ya kutaka wajumbe wenzao wawaelewe vyema huwalazimu kuteua Kiswahili wakati wa mjadala bungeni.

4.2.10 Hotuba kwa Wananchi Katika Lugha ya Kiswahili

Kauli hii ilionekana kuwachangamsha wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya kwani asilimia kubwa ya sabini nukta tatu saba (70.37%) walikubaliana vilivyo nayo. Wajumbe hawa walidai kuwa kuingia kwao bungeni hutegemea maelewano yao na wananchi wapiga kura na hivyo basi hawana budi kuwaelezea sera zao kwa lugha wanayoelewa zaidi. Walidai kuwa hii ndiyo lugha wanayotumia kuomba kura kwa wapiga kura na hivyo basi takribani hotuba zao zote wao huamua kutumia Kiswahili. Hata hivyo asilimia ya ishirini na tisa nukta sita tatu (29.63%) ya wajumbe waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa wao huwakilisha wodi za mijini kuliko na wapiga kura kutoka nje ya siaya na hata nje ya taifa la Kenya na wao huwa na ugumu wa kuelewa Kiswahili. Hili huwalazimu labda kutumia lugha za kigeni na haswa Kiingereza. Pia wengine wao walieleza kuwa wanawakilisha wodi za mipakani kuliko na makabila tofauti na hivyo wao hulazimikaa

kuhutubia kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na kiingereza kwa mapana. Kunao waliodai kuwa vijijini kwao kuna wasomi wachache na hivyo huwabidi kuchanganya lugha ya Kiswahili na zile za mama ili kufikisha ujumbe kwa wananchi vyema.

Jedwali 12: Napenda Kuwahutubia Wananchi ninaowakilisha kwa Kutumia Lugha ya Kiswahili

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 19 | 70.37 | 8 | 29.63 | 27 | 100 |

Kwa mujibu wa matokeo ya kauli hii ni kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walipendelea mno kutumia lugha ya Kiswahili wanapowahutubia wananchi wanaowakilisha ili kuelewana nao vilivyo. Hii ni ishara tosha kuwa wengi wa wajumbe wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwa vile wangependa kuwasiliana na wapiga kura wao kwa lugha wanaoelewana nayo. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwani matarajio ya jamii wanamotoka wajumbe husika huwalazimu kuwa na mielekeo ya kuchangua Kiswahili katika mawasiliano.

4.2.11 Uamuzi wa Kuchagua baina ya Kiingereza au Kiswahili katika Mazungumzo

Matokeo ya kauli hii yalidhihirisha wazi kuwa asilimia kubwa ya themanini na nane (88.89%) ya wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya huegemea kwenye Kiswahili pindi wanapojipata kwenye mwanya wa kufanya maamuzi kati ya lugha ya kutumia kati ya Kiswahili na Kiingereza. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiswahili ndiyo lugha pana ya mitaani na hivyo huingia akilini kwa haraka ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Pia wajumbe waliokuwa na mtazamo chanya kuhusiana na kauli hii walieleza kuwa watu wengi kwenye jimbo la Siaya walienzi Kiswahili na hivyo basi uamuzi wa kukitumia ulijitokeza moja kwa moja. Baadhi ya asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) ya wajumbe waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa wanawakilisha wananchi wa wodi za mijini kuliko na wasomi wanaojivunia lugha za kigeni. Hili huwalazimu

wajumbe hawa mara nyingi kuchagua Kiingereza badala ya Kiswahili hali hii inapohitajika kwao.

Jedwali 13: Huchagua Kiswahili kila mara Ninapokabiliwa na Uamuzi wa Kuchangua Kutumia Lugha ya Kiingereza au Kiswahili

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 24 | 88.89 | 3 | 11.11 | 27 | 100 |

Matokeo ya kauli hii yaliashiria wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hupenda Kiswahili na iwapo wanatakiwa kufanya maamuzi ya kuchangua kati ya lugha hii na kiingereza, wao huegemea lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, wajumbe wengi wana mielekeoa chanya kuhusiana na kauli hii kwa vile kwao Kiswahili kina mashiko sana na hivyo endapo kuna nafasi ya kuchangua lugha ya matumizi wao hukichangua bila pigamizi. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa kwani wajumbe husika wana sababu maalumu ya kuteua lugha fulani dhidi ya nyingine.

4.2.12 Hisia Chanya wakati wa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Bungeni

Idadi ya wajumbe waliokubaliana na kauli hii walikuwa asilimia themanini na moja nukta nne nane (81.48%) hali iliyodhihirisha wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya huwa hawana haya wanapotumia lugha ya Kiswahili bali hujivunia na lugha hii ya taifa. Wajumbe hawa walieleza kuwa kwa vile wao ni wakenya halisi wanajivunia kwa lugha ya Kiswahili iliyo na dhima ya kuwaunganisha wakenya na hivyo hujihisi mashujaa wanapotumia lugha hii wakati wa kutoa hoja zao bungeni. Ushujaa huu unadhihirika wanapotumia misamiati mizito mizito na mbinu za lugha zenye uzito wa hali yake kusukuma ujumbe uliotengenezewa akilini. Hata hivyo kuna asilimia kumi na nane nukta tano mbili (18.52%) iliyokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii. Wajumbe kwenye kitengo hiki walidai kuwa Kiswahili sio lugha ya kujivunia nayo kwani msambao wake ulimwenguni ni duni. Walidai kuwa kujivunia na lugha ya Kiswahili ni kinaya kwani watembeleapo

mataifa ya ng'ambo hufedheheka wanapong'ang'ana kutafuta misamiati ya Kiingereza ili kuwasiliana na wazungu.

Jedwali 14: Hujihisi kuwa Shujaa Ninapotumia Kiswahili katika Mijadala Bungeni

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 22 | 81.48 | 5 | 18.52 | 27 | 100 |

Matokeo ya kauli hii yalihariri ukweli kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hujihisi mashujaa wakubwa wanapotumia lugha ya Kiswahili bungeni. Ushujaa huu unatokana na mapenzi ya Kiswahili kwa mioyo ya dhati. Kauli hii inadhihirisha kuwa wengi wa wajumbe wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli husika kwani ufasaha wa lugha ya Kiswahili kwao huwafanya mashujaa wa utumizi wa misamiati yenye mnato wa kweli. Kauli hii inadhihirisha kuwa wengi wa wajumbe wana mielekeo chanya kuhusiana na kauli husika kwani ufasaha wa lugha ya Kiswahili kwao huwafanya mashujaa wa utumizi wa misamiati yenye mnato wa kweli. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuisho wa Utambulisho kwa vile wajumbe husika hupendelea lugha ya Kiswahili ili wajihisi mashujaa.

4.2.13 Utazamaji Vipindi vya Televisheni katika Lugha ya Kiingereza

Asilimia kubwa ya sitini na sita nukta sita saba (66.67%) ya wajumbe wa kaunti ya Siaya walionekana kuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii. Wajumbe hawa walieleza kuwa lugha ya Kiingereza mara nyingi huwa na lafudhi nzito isiyoeleweka kwa urahisi na hivyo kuwakanganya wanapotazama vipindi vya Kiingereza. Wengine walidai kuwa familia zao hupendelea kusikiliza na kutazama vipindi vinavyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili kwani ndiyo lugha inayoeleweka vyema na haswa watoto. Maswali mengi kutoka kwa watoto wao huwalazimu kufuatilia vipindi vya lugha ya Kiswahili ili kuondoa hatihati nyumbani. Wajumbe walioonekana kukubaliana na kauli hii kwa

asilimia thelathini na tatu nukta tatu tatu (33.33%) walidai kuwa wao waliendeleza masomo yao ya juu ng'ambo na hivyo kukienzi Kiingereza kuliko Kiswahili. Pia walidai kuwa wao huchukua muda wao kutazama vipindi vya Kiingereza kwenye simu zao telezi na hivyo basi kusawazisha hamu hii kwenye vipindi vya lugha hii ya kigeni kwenye runinga.

Jedwali 15: Hupenda Kutazama Vipindi vya Televisheni katika Lugha ya Kiingereza

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|----------|--------------|-----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 9 | 33.33 | 18 | 66.67 | 27 | 100 |

Matokeo ya kauli hii ni kuwa wajumbe wengi hawana moyo wa kutazama vipindi vya lugha ya Kiingereza kwenye televisheni kwa sababu zao za kibinafsi. Kwa kuwa na mitazamo hasi ya lugha hii ya kigeni, wajumbe hawa walikuwa na chuki na vipindi vya Kiingereza. Hii ina dhibitisho kuwa wengi wa wajumbe wa jimbo la Siaya wana mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwa vile vipindi vya Kiswahili kwenye runinga huwa na mnato wake kwao na familia zao. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa vile wajumbe wanakwazwa na lugha ya kiingereza inayoleta vipindi katika televisheni.

4.2.14 Ujasiri wa kuzungumza Kiswahili

Wajumbe wengi walikubaliana na kauli hii kwa asilimia sabini na nne nukta sufuri saba (74.07%) kwa kudai kuwa hawawezi kujihisi wanyonge wanapoongea Kiswahili kwani ni jukumu lao kulinda katiba kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Walidai kuwa katiba ya Kenya iliyoweka Kiswahili kuwa lugha ya kitaifa, waliapa kuilinda kwa vyovyote vile na hivyo basi kujihisi wanyonge wanapoongea lugha hii utakuwa usaliti mkubwa kwa katiba yao. Kuna asilimia ishirini na tano nukta tisa tatu (25.93%) ya wajumbe iliyodai kuwa hujihisi kuwa na unyonge wanapoongea Kiswahili kwani ni lugha ya eneo dogo tu la Afrika Mashariki na hivyo basi kujivunia nayo ni kuwa na mtazamo finyu

kuhusu utembezi wa ulimwengu na lugha nyingine za dunia.

Jedwali 16: Nikiongea Kiswahili huwa Sijihisi Mtu Mnyonge

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 20 | 74.07 | 7 | 25.93 | 27 | 100 |

Wajumbe wengi wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani hawajioni na unyonge wowote wakati wa kutumia Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa kuwa kupendelea lugha ya Kiswahili inawapa ukakamavu wa kujihisi kuwa sio wanyonge kwa vyovyote vile.

4.2.15 Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili Fasaha

Asilimia kubwa ya themenini na moja nukta nne nane (81.48%) ya wajumbe wa kaunti ya Siaya walionekana kukubaliana na kauli hii ya kuwa na ujuzi wa kupendelea kuwa na ujuzi na umilisi wa kuzungumza Kiswahili fasaha. Walieleza kuwa ujuzi na umilisi wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha, kutawafungulia milango mingi ya kuelimisha watoto wao na pia jamii zao kuhusu ubora wa mali asilia za Afrika. Pia ujuzi na umilisi huu utawapa nafasi ya kutoa hoja za mijadala yao bungeni bila kusitasita. Wajumbe waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii kwa asilimia kumi na nane nukta tano mbili (18.52%) walidai kuwa ujuzi na umilisi huu utakosa faida kwao kwani jamii za mijini wanaotangamana nazo hazijivunii lugha ya Kiswahili ila ile ya Kiingereza.

Jedwali 17: Ningepeda niwe na Ujuzi na Umilisi wa Kuzungumza Kiswahili kwa Ufasaha

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 22 | 81.48 | 5 | 18.52 | 27 | 100 |

Matokeo yaliyotokana na kauli hii yalidhihirisha wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya

hawajihisi wakiwa na unyonge wowote wanapoongea lugha ya Kiswahili ndani na nje ya bunge. Hii ni kutokana na hali kuwa hii siyo lugha ya kitaifa pekee bali pia ni lugha ya kimataifa inayoenziwa dunia nzima. Wajumbe wengi wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani hawajioni kuwa na unyonge wowote wakati wa kutumia Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa kuwa wajumbe wengi wana matarajio ya kibinafsi ya kuwa na ujuzi na umilisi wa lugha ya Kiswahili.

4.2.16 Kiswahili ni Lugha inayohitaji Ufasaha kwa wingi

Matokeo ya kauli hii yalionyesha kuwa asilimia kubwa ya themanini na nane nukta nane tisa (88.89%) ya wajumbe wa kaunti ya Siaya ilionekana kukubaliana na kauli ya kuwa Kiswahili ni lugha yenye ufasaha kwa wingi. Kwa kukubaliana na kauli hii, wajumbe walidai kuwa kuwepo kwa maandishi rejelewa mengi ya Kiswahili yakiwemo vitabu na kamusi za Kiswahili husheheni misamiati kwa wingi iliyo na ufasaha mwingi. Vilevile, walidai kuwa kuna walimu wenye tajriba kubwa ya lugha ya Kiswahili na hivyo basi kuelekeza wanafunzi wao kwenye uwanja huu wa ufasaha wa lugha. Hata hivyo, wajumbe waliokuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii kwa asilimia kumi na moja nukta moja moja (11.11%) walidai kuwa Kiswahili kimepungukiwa na ufasaha kwani ni lugha inayokua na kubadilika siku baada ya siku. Ukuaji na ubadilikaji huu hunyima lugha ya Kiswahili ufasaha wake kwani hukosa ustadi wa ufasaha wa daima.

Jedwali 18: Kiswahili ni Lugha yenye Ufasaha kwa wingi

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 24 | 88.89 | 3 | 11.11 | 27 | 100 |

Kwa mujibu wa matokeo ya hojaji za wajumbe wa Siaya ni kuwa zaidi ya asilimia themanini ya wajumbe walikuwa na mitazamo chanya kuhusiana na ufasaha ulio kwenye lugha ya Kiswahili. Ni

wachache mno waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii. Mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii ni thibitisho tosha kuwa wengi wa wajumbe wanajua lugha ya Kiswahili kama iliyo na ufasaha mwingi kwani ina misamiati kwa wingi. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa kwa vile sababu moja ya kupendelea Kiswahili dhidi ya lugha nyingine ni kuwa ni lugha yenye ufasaha kwa wingi.

4.2.17 Utazamaji wa Vipindi vya Televisheni katika Kiswahili

Kauli hii ilionekana kukataliwa na wajumbe wengi kwa asilimia sabini nukta tatu saba (70.37%) kwa kudai kuwa wao hupenda kusikiliza vipindi vya televisheni katika Kiswahili. Wajumbe wengi walidai kuwa wao hawachukii kusikiliza vipindi vya televisheni katika Kiswahili kwani lugha hii huwa na misamiati na mbinu za lugha za kuchangamsha wasikilizaji na hivyo kuwachekesha na hivyo basi wanapendelea kusikiliza vipindi hivyo. Asilimia ya wajumbe waliokuwa na mtazamo wa kukubaliana na kauli hii walikuwa asilimia ishirini na tisa nukta sita tatu (29.63%) na ambao walidai kuwa vipindi vya Kiswahili vimepungukiwa na ubunifu na hivyo basi wao huchukia kuvisikiliza. Wao hupendelea kusikiliza vipindi vilivyobuniwa kwa lugha za kigeni na za lugha za mama.

Jedwali 19: Nachukia kusikiliza Vipindi vya Televisheni katika Kiswahili

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|----------|--------------|-----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 8 | 29.63 | 19 | 70.37 | 27 | 100 |

Matokeo ya kauli hii yalidhihirisha kuwa wajumbe wengi wa kaunti hii ya Siaya hawakubaliana na kauli hii na hivyo basi ni ishara tosha kuwa vipindi vinanyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili ni kipenzi chao. Wajumbe wengi wana mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwani hawawezi kuchukia lugha inayoenziwa na wananchi wanaowakilisha. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa kuwa wajumbe wengi hawakubani na vikwazo wasikizapo vipindi kwa

luga ya Kiswahili.

4.2.18 Matumizi ya Kiswahili katika Mazingira ya Kazi

Asilimia kubwa ya themanini na moja nukta nane (81.48%) ya wajumbe wa kaunti ya Siaya ilionekana kuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii kwa kudai kuwa Kiswahili ni lugha ya kuunganisha wakenya na hivyo basi inapaswa kudumishwa kwenye ofisi za serikali na mazingira ya kazini. Walidai kuwa Kiswahili ni lugha rahisi kwa raia wengi na hivyo kuipiga marufuku kwenye mazingira ya ofisini na kazini itakuwa pigo kubwa kwao. Asilimia kumi na nane nukta tano mbili (18.52%) ya wajumbe waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa taifa la Kenya ni nchi inayovutia wananchi kutoka mataifa mbalimbali wasiokuwa na ufahamu wa Kiswahili. Walidai kuwa lugha za kigeni zinapaswa kutumiwa kwenye mazingira ya ofisini na kazini ili kuvutia wageni walio na ujuzi mkubwa katika sekta nyingi za ujenzi wa taifa.

Jedwali 20: Matumizi ya Kiswahili yanapaswa Kupigwa Marufuku kwenye Mazingira ya Kazini

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 22 | 81.48 | 5 | 18.52 | 27 | 100 |

Matokeo yaliyotokana na hojaji zilizojazwa kuhusiana na kauli hii yalidhihirisha wazi kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya hawakukubaliana na kauli hii. Waliashiria kuwa kuwepo kwa matumizi ya Kiswahili kwenye mazingira ya ofisini na kazini kuna manufaa makubwa kwa walioko kule. Hivyo basi wengi wa wajumbe wanaonekana kuwa na mielekeo hasi kuhusiana na kauli hii kwani hawawezi kubali lugha ya taifa kutupiliwa mbali katika ofisi za serikali Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa kuwa kulingana nao hakuna vikwazo vya matumizi ya Kiswahili katika ofisi na mazingira ya kazi.

4.2.19 Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Kitaifa

Wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walionekana kuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii kwa

asimia themanini na moja (81%) kudai kuwa Kiswahili ni lugha iliyovuka mipaka ya kimataifa na hivyo basi haiwezi kuwa duni. Wajumbe hawa walidai kuwa Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kiafrika na hivyo basi kuichukulia kama lugha duni itakuwa kudunisha bara hili na kukweza mabara ya nje. Hii itakuwa kinyume na mwito wa waafrika kujivunia na utamaduni wao asilia. Wajumbe wengine waliopinga kauli hii walidai kuwa lugha ya Kiswahili haiwezi kuwa duni kwani imetumika kwenye mazingira ya taasisi za elimu, kwenye nyanja za siasa ikiwemo bungeni na pia kwenye mazingira ya sekta za ujenzi wa taifa na umuhimu wake kushuhudiwa wazi. Hata hivyo, wajumbe walioonekana kukubaliana na kauli hii kwa asilimia kumi na tano (15%) walidai kuwa kuzidi kuienzi lugha ya Kiswahili ni kurudisha taifa la Kenya nyuma. Hii ni kwa sababu ulimwengu wa utandawazi unazidi kupanuka kila uchao na lugha tumikizi kule ni za kigeni. Walidai kuwa Kiswahili kinazidi kupitwa na wakati na haswa katika taasisi za elimu kwani mitandao nyingi hutumia lugha za kigeni na itakuwa vigumu kuzitafsiri kuzileta kwa Kiswahili.

Jedwali 21: Kiswahili ni Lugha Duni na Isiyopaswa Kulazimishwa Itumike Kitaifa

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|----------|--------------|-----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 5 | 18.52 | 22 | 81.48 | 27 | 100 |

Kwa mujibu wa matokeo ya kauli hii ni dhahiri kuwa wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walionekana kupinga kauli hii kwani kulingana nao hii ni lugha kama lugha nyingine duniani na kuwa mitazamo ya Waafrika ndio walio na maoni duni mbali sio Kiswahili. Hivyo basi, wengi wa wajumbe wanaonekana na mielekeo hasi kwani Kiswahili hakiwezi kuwa duni ilhali ni lugha kimataifa. Kauli hii inapingwa na nadharia ya Ujumuishi wa Utambulisho kwa kuwa wao hawaoni vikwazo vya Kiswahili kuzidi kuwa lugha ya kutumika kitaifa.

4.2.20 Kiswahili kama Chombo cha Umoja wa Wakenya

Asilimia kubwa ya sabini na nane (78%) ya wajumbe wa kaunti ya Siaya walionekana kukubaliana na kauli hii ya Kiswahili kuwa chombo cha umoja wa Wakenya. Walieleza kuwa taifa la Kenya lina makabila Zaidi ya arobaini na hivyo Kiswahili kufanywa kuwa chombo cha umoja ni mojawapo wa hatua yenye umuhimu mkubwa uliofanywa na serikali ya Kenya. Walieleza kuwa makabila yakiwa na ufahamu huu yatajifunga kibwebwe kujifunza lugha hii ya taifa. Waliokuwa na mtazamo hasi kuhusiana na kauli hii walikuwa asilimia kumi na tano (15%) na ambao walidai kuwa taifa la Kenya sio nchi ya Wakenya pekee mbali ina wageni kutoka mataifa mengi duniani wasiofahamu Kiswahili. Walidai kuwa umoja unaohitajika wa wageni hawa na Wakenya asilia utakuwa wa kutilia shaka endapo taifa la Kenya litazidi kupalilia Kiswahili kama chombo cha umoja huu. Hivyo basi walipendekeza lugha nyingi kutambuliwa kwenye katiba kuwa vyombo vya umoja wa Wakenya.

Jedwali 22: Kiswahili ni Chombo cha kuwaunganisha Wakenya

| | Ndio | Asilimia | La | Asilimia | Jumla | Asilimia |
|---------|-----------|--------------|----------|--------------|-----------|------------|
| Wajumbe | 21 | 77.78 | 6 | 22.22 | 27 | 100 |

Matokeo ya hojaji ya wajumbe wa Siaya yalionyesha kuwa wajumbe wengi walikuwa na mitazamo kubalifu ya kuwa Kiswahili ni chombo cha umoja wa Wakenya kwani ni lugha iliyoenea kote nchini. Hivyo basi, wengi wa wajumbe wanaonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusiana na kauli hii kwani jamii ya Kenya imeshuhudia muungano ulio wazi unaoletwa na Kiswahili. Kauli hii inaungwa mkono na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa kwa vile wajumbe husika wanatarajia Kiswahili kuleta umoja wa kitaifa.

4.3 Hitimisho

Katika sura ya nne, kauli za mielekeo ya wajumbe kuhusu uteuzi wa lugha ziliangaziwa kwa undani

wake. Vilevile, sababu za wajumbe kuwa na mtazamo fulani zilichanganuliwa kwa lengo la kusoma akili za wajumbe wa kaunti ya Siaya. Vielelezo pamoja na majedwali kuhusiana na vipengele vya kauli na sababu za mielekeo ya wajumbe zimechorwa katika sura hii.



SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulinuia kuchunguza mielekeo ya wajumbe katika uteuzi wa lugha ya mijadala bungeni katika kaunti ya Siaya. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kuchunguza iwapo mielekeo inachangia uteuzi wa lugha inayotumika katika mijadala ya wajumbe bungeni, kuchambua iwapo wajumbe wa bunge la kaunti ya Siaya wana sababu maalumu zinazowapelekea kuchagua lugha moja dhidi ya nyingine katika mijadala bungeni, kuchunguza iwapo kuna lugha mahususi inayopendelewa na wajumbe katika mijadala ya bungeni na kuchunguza iwapo kuna vikwazo vinavyowazuia wajumbe wa kaunti ya Siaya kutumia Kiswahili kufanikisha mawasiliano katika muktadha wa mijadala bungeni. Ili kuafikia malengo ya utafiti huu, Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Nadharia Jumuishi ya Utambulisho ziliweza kuongoza utafiti huu. Katika sura hii ya tano, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti, mapendekezo yake pamoja na hitimisho la utafiti zimejadiliwa.

5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulichukua sura tano. Sura ya kwanza ilijadili vipengele vya msingi vya utafiti vikiwemo usuli wa mada, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, mawanda na mipaka ya mipaka utafiti pamoja na maelezo ya istilahi muhimu zilizotumika. Katika sura ya pili, yaliyoandikwa kuhusu mada pamoja na misingi ya nadharia ziliangaziwa. Sura ya tatu ilijadili kuhusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na uteuzi wa sampuli, mbinu na vifaa vya kukusanya data, uchambuzi na uwasilishaji wa data pamoja na maadili ya utafiti.

Katika sura ya nne, vipengele vya uchanganuzi wa kauli za mielekeo kulingana na wajumbe pamoja na sababu za mielekeo ya wajumbe kuhusu uteuzi wa lugha zilijadiliwa.

Hatimaye, sura ya tano imeangazia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, vikwazo vya utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti.

Utafiti huu ulikuwa na kauli ishirini ambapo wajumbe walikuwa na nafasi ya kutoa maoni yao kuhusiana na kauli husika. Ilibainika kuwa wajumbe wa kaunti ya Siaya wana mielekeo tofauti kuhusu mielekeo ya uteuzi wa lugha inayopaswa kutumika katika mijadala ya bungeni. Kuna waliokuwa na mitazamo chanya kuhusiana na kauli fulani huku wengine wakiwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli ile ile. Kwa jumla kila mtazamo uliandamana na sababu zake na hivyo mtafiti kuwa na nafasi ya kusoma akili za wajumbe kuhusu mielekeo yao ya uteuzi wa lugha.

Katika kauli ya kwanza, wajumbe wengi wa kaunti ya Siaya walionekana kukubaliana na kauli ya kuwa ni rahisi kujifunza Kiswahili kwani ni lugha ya taifa na ya shuleni. Asilimia ya chini mno ya wajumbe waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa Kiswahili huwa na matamshi magumu ambayo hutatiza kutamkwa. Katika kauli ya pili, wajumbe wengi walionekana na mitazamo chanya kwa kupenda kutumia Kiswahili kutoa hoja zao katika mijadala ya bungeni kwani wanakienzi tangu shuleni. Waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa hawapendi kutumia Kiswahili kwani matamshi yake huwatatiza na hivyo kuogopa kuchekwa na wenzao.

Wajumbe wengi walikubaliana na kauli ya tatu ya kukiri kuwa wajumbe wenzao huelewa ujumbe zaidi wanapotumia Kiswahili kwani ndio lugha inayozungumzwa na watu wengi. Hata hivyo waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa kuna wajumbe waliosomea ng'ambo na hivyo huwa vigumu kwao kuelewa vyema ujumbe kwa Kiswahili. Kauli ya kuwa lugha ya Kiswahili ina dhima kubwa kwa maendeleo ya taifa la Kenya ilikubaliwa na wajumbe kadhaa waliodai kuwa ni lugha unganishi na hivyo kutumiwa na raia wengi kwenye sekta nyingi za ujenzi

wa taifa. Waliokuwa na mitazamo hasi ya kauli hii walidai kuwa maendeleo mengi hutoka kwa wageni kutoka nje mwa Kenya na ambao hawaelewi Kiswahili. Wajumbe wengi walikuwa na mitazamo chanya kuhusiana na kauli ya sita ya kufurahishwa na kuchangamshwa na vipindi vya Kiswahili kutoka vyombo vya habari kwani misamiati ya Kiswahili huwa na vichekesho kwa wingi. Hata hivyo, waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa vipindi vya Kiswahili vimepungukiwa na ubunifu na hivyo hawavipendi.

Kauli ya sita ilikataliwa kwa kiasi kikubwa na wajumbe kwa kudai kuwa wanasiasa wengi katika kaunti ya Siaya hawapendelei kutumia Kiingereza katika mijadala ya bungeni kwani huwa lugha ngumu kwao. Wachache waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa wako sawa na Kiingereza kwani walisomea ng'ambo na kuenzi lugha hii ya Mkoloni. Kauli ya saba ilionekana kukataliwa na wajumbe wengi kwa kudai kuwa wanapofanya mazoezi, uzungumzi wa Kiswahili huja kwa urahisi kwao. Hata hivyo, waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa kwao Kiswahili huwasumbua hata wakifanya mazoezi kwa kiasi fulani na hili huwavunja moyo wa kuzungumza lugha hii ya taifa. Kauli ya nane ilikataliwa na wajumbe wengi kuwa wajumbe wenzao hawana nafasi ya kuwacheka kwani wameiva kwa lugha ya Kiswahili na hivyo matamshi yao huwa sawa. Waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa wao huchekwa kwani wamebomba kuzungumza kwa Kiingereza kuliko Kiswahili.

Wajumbe wengi walisema kuwa wao hupenda kuchanganya lugha haswa wanapokumbana na maneno mazito yasiyoeleweka kwa Kiswahili na Kiingereza. Waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa wao hawahitaji kuchanganya lugha kwani wameboba kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza na wanaweza kusema lugha hizi kwa mfululizo. Wajumbe wengi walionekana kuwa na mitazamo kubalifu kuhusiana na kauli ya kumi kwa kuwahutubia wananchi kwa Kiswahili. Kisa na maana, hii ndiyo lugha inayozungumzwa na raia wengi na hivyo ndio lugha ya kufikisha ujumbe kwao ili waeleweke vyema. Waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli

hii walidai kuwa wao huwakilisha wodi za jijini na hivyo inabidi kwao kutumia Kiingereza kwani wengi wa wakaazi kule ni wasomi. Wengine walidai kutumia lugha za mama kwani kule mashinani wananchi wengi wana elimu ya kiwango cha chini na hivyo kushindwa kuelewa Kiswahili vyema.

Kauli ya kumi na moja ilikubaliwa na wajumbe wengi walioidai daima wao huchagua Kiswahili kuliko Kiingereza endapo haja hiyo itazuka. Hii ni kwa sababu Kiswahili ndio lugha rahisi kwao na hivyo huja ulimini kwa urahisi. Wachache waliokana kauli hii walidai kuwa Kiingereza ndio lugha ya karibu nao kwani walisomea ng'ambo na hivyo wao huichagua haja hiyo inapozuka. Asilimia kubwa ya wajumbe ilionyesha kuwa wao hujihisi mashujaa wanapotumia Kiswahili katika mijadala kwani ni lugha ya taifa iliyo na misamiati changamfu. Waliojihisi wanyonge walidai kuwa hawawezi kujihisi mashujaa kwa lugha ya eneo dogo la Afrika Mashariki na wao hupenda lugha za kimataifa.

Wajumbe kadhaa walionekana kuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli ya kuwa wao hupenda kutazama vipindi vya Kiingereza katika televisheni. Kwao Kiingereza na lugha ya kigeni isiyo na misamiati ya kuchangamsha. Waliokubaliana na kauli hii walisema kuwa vipindi vya Kiingereza huwa na ubunifu wa hali ya juu na hivyo wao hupenda kuvitazama. Wajumbe wengi walionekana kukubaliana na kauli ya kumi na mne kwa kudai kuwa hawajihisi wanyonge wanapotumia Kiswahili kwani ni lugha ya taifa na wao hujivunia kuwa wakenya. Waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa wao hujihisi wanyonge kwani Kiswahili ni lugha ya eneo dogo na wao hupendelea lugha za kigeni ambazo mawanda yake ni mapana.

Kauli ya kumi na tano ilikubaliwa na wajumbe wengi kwa madai kuwa ujuzi na umilisi wa lugha ya Kiswahili huwasaidia sana haswa wanapotoa hoja za mijadala bungeni. Waliokuwa na mitazamo ya kukataa kauli hii walidai kuwa hawana haja ya kuwa na ujuzi na umilisi wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha kwani ni lugha duni kwao isiyoeleweka kwenye mataifa ya ng'ambo. Kauli ya kuwa

Kiswahili huwa lugha yenye ufasaha kwa wingi ilikubaliwa na wajumbe wengi waliodai kuwa kuna maandishi mengi ya lugha hii na hivyo kupanua ufasaha wake kwa wanafunzi na wazungumzaji wake. Hata hivyo, waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa ufasaha wa Kiswahili ni wa kiwango cha chini mno kwani utandawazi unazidi kupanuka na hivyo kuwa na haja ya kutafuta misamiati mpya ya maneno na istilahi za mitandao.

Kauli ya kumi na saba ilikataliwa na idadi kubwa ya wajumbe waliodai kuwa wao hawachukii kusikiliza vipindi vya televisheni katika Kiswahili kwani ndio lugha iliyo na misamiati na mbinu za lugha zenye vichekesho kwa wingi. Waliodai kuwa wanachukia vipindi vya Kiswahili walisema kuwa vipindi hivi vimepungukiwa na ubunifu na hivyo wao huvichukia kwa dhati. Kauli ya kumi na nane ilikataliwa kwa kiasi kikubwa cha wajumbe waliodai kuwa kupiga marufuku matumizi ya Kiswahili kwenye mazingira ya ofisi na kazini litakuwa pigo kubwa kwa wananchi wasioelewa Kiingereza. Pia walidai kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa na hivyo ndio lugha inayopaswa kutumiwa kazini ili kusaidia katika ujenzi wa taifa. Waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa kusifu Kiswahili ofisini na kazini ni kufukuza wageni walio na ujuzi wa hali ya juu kwenye sekta mbalimbali na wasiojua lugha ya Kiswahili.

Kauli ya kumi na tisa ilikataliwa na asilimia kubwa ya wajumbe waliodai kuwa Kiswahili ni lugha ya Mwafrika na hivyo haiwezi kuwa lugha duni. Walidai kuwa Waafrika wanapaswa kujivunia na mali yao asilia na sio kusifu lugha za wageni. Wajumbe wachache waliokubaliana na kauli hii walidai kuwa Kiswahili ni lugha duni kwani mawanda yake ni finyu mno maana inapatikana Afrika Mashariki pekee.

Hatimaye, asilimia kubwa ya wajumbe walikuwa na mitazamo kubalifu ya kauli ya ishirini kuwa Kiswahili ni chombo cha umoja wa Wakenya. Kisa na maana, hii ni lugha ya taifa na hivyo basi

hutumika kama kiunganishi cha makabila zaidi ya arobaini nchini Kenya. Hata hivyo, wajumbe wachache waliokuwa na mitazamo hasi kuhusiana na kauli hii walidai kuwa taifa la Kenya sio la Wakenya pekee bali lina wageni wasiojua wala kuelewa Kiswahili na hivyo umoja wao unapuuzwa pale ambapo Kiswahili kitachukuliwa kama chombo cha umoja wa Wakenya.

5.2 Vikwazo vya Utafiti

Mtafiti alikumbana na vikwazo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data za utafiti huu. Katika harakati za ukusanyaji wa data, kuna baadhi ya wajumbe ambao walichukua muda mwingi kujaza fomu za hojaji walizopewa. Kuna wajumbe wengine waliopewa fomu za hojaji lakini wakakosa kurudisha na hivyo mtafiti hakujua kama walijaza zile fomu au walipuuza mwito wa mtafiti. Vile vile, baadhi ya wajumbe walikuwa kwenye likizo za kibinafsi na hivyo ikabidi mtafiti kuwa na subira. Wajumbe wengine walikuwa na kazi nyingi kwa hivyo mara nyingi ilimlazimu mtafiti kufuata ratiba yao ili wajaze fomu za hojaji labda wakati wa mapumziko. Hatimaye, mtafiti alikumbana na kikwazo cha kifedha kwani subira yake kwa wajumbe ilizidisha muda aliokuwa amepangia kuwoko kwenye maeneo ya bunge la Siaya. Hata hivyo, wingi wa vikwazo alivyokumbana navyo mtafiti havikuathiri pakubwa utafiti huu.

5.3 Mapendekezo ya Mtafiti

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ya mtafiti na ambayo ana imani kuwa yatakuwa na manufaa kwa serikali za ugatuzi, wakufunzi kwenye taasisi za elimu na pia watafiti wengine wa baadaye na ambao watakuwa na nia ya kutafitia mada ya mielekeo ya uteuzi wa lugha kwenye nyanja mbalimbali za serikali na za kibinafsi.

Kwanza, ili kuwe na msimamo sawia wa lugha inayohitajika kutumiwa katika mijadala kwenye mabunge ya kaunti za Kenya, wajumbe wanapaswa kupewa nafasi za kuhudhuria warsha za lugha za

Kiswahili na Kiingereza ili kunoa makali ya matumizi ya lugha moja kwa mfululizo inapohitajika. Pili, taasisi zote za elimu nchini Kenya kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu zifanye lugha za Kiswahili na Kiingereza kuwa masomo ya lazima na ya kutahiniwa ili wanafunzi wazidi na kuyatilia maanani masomo haya. Hili litawalazimu wanasiasa kunoa makali ya matamshi ya maneno kwenye lugha zote mbili.

Pendekezo la tatu ni kuwa katiba inapaswa kubadilishwa ili iwe na kipengele cha sheria kuwa lazima kila Mkenya anayetaka kujitosa kwenye ulingo wa siasa awe na kiwango cha elimu hadi chuo kikuu. Hili litawafanya wanasiasa hawa kuiva kwenye uwanja wa lugha.

Pendekezo la nne ni kuwa utafiti huu unaweza kufanywa kutoka vitabu vya fasihi vikiwemo riwaya, tamthilia na ushairi. Hili litapanua mawanda ya uchunguzi kuhusu mielekeo ambayo hudhibiti uteuzi wa lugha fulani kwenye taasisi tofauti.

Pia, serikali inapaswa kuwapitisha walimu wa lugha waliohitimu kwenye masuala ya lugha katika warsha mbalimbali ili wazidi kujifahamisha kuhusu mabadiliko na ukuaji wa lugha unaozidi kushuhudiwa kila uchao. Hili litawapa walimu hawa ufahamu zaidi wa lugha watakaopitisha kwa wanafunzi wao ili kunoa makali yao ya matamshi.

Pendekezo jingine ni kuwa utafiti wa suala kama hili unaweza kufanyika kwenye kaunti nyingine iliyo tofauti na aliyotafitia mtafiti. Hili litasaidia kulinganisha mielekeo ya uteuzi wa lugha kutoka jimbo moja hadi jingine.

Hatimaye, mtafiti anapendekeza kuwa wajumbe wanaotumia lugha moja mfululizo na kwa ufasaha katika mijadala watuzwe ili kutia wengine ari ya kupenda na kujifunza lugha wanayoipenda.

5.4 Hitimisho

Katika sura hii ya tano, mtafiti alishughulikia utangulizi wa sura, muhtasari wa matokeo ya utafiti na vikwazo vya utafiti. Zaidi ya hayo mtafiti ametoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye ambao wangukuwa na kusudi la kutafitia kuhusu mada inayohusiana na mielekeo ya lugha.



MAREJELEO

- Adegbija, E. (1994). *Language attitudes in Sub-Saharan Africa: A sociolinguistics overview*. Clevedon, England: Multilingual Matters.
- Agheysi, R. & Fishman, J. (1970). A language attitudes survey studies: A brief survey of methodological approaches. In *Anthropological Linguistics*. 7(2):321.
- Ajzen, I. (1991). *The theory of planned behaviour: Organization behaviour and human decision processes*. Inglewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall
- Ajzen, I. & Fishbein, M. (1980). *Understanding attitudes and predicting social behaviour*. Inglewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall
- Ali, J.N. (2011). *Changamoto zinazokumba mawasiliano ya kiofisi kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi*.
- Babusa, H.O (2010). *Uchanganuzi wa lugha wa mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili wa wanafunzi katika mkoa ya Pwani na Nairobi nchini Kenya*. Kenyatta University PhD D Thesis
- Batibo, H.H. (2005). *Language decline and death in Africa: Causes, consequences and challenges*. Clevedon: Multilingual Matters
- Bourhis, Y.R. (1982). *Language Policies and Language Attitudes. Attitudes towards Language Variation*. London. Edward Arnold Publishers.
- Brudner, L.A & White D (1979). *Language Attitudes Blair & Intervening Variables Katika Mackay W.F(ed). Sociolinguistics Studies in Context Methods and Cases*. The Haggish Mouton Publishers.

Canale, M & Swain M. (1980). *Theoretical Bases of Communicative Approaches to Second Language Teaching and Testing in Applied Linguistics*.

Chieni S.N (2001). *Language and Society: Kiswahili National Language of Social Class Language in Kenya*. Shitemi N and Mwakombo M.N Moi University Press.

Chimerah, R. (1998). *Kiswahili past present and future horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.

Creswell, J.W (2003). *Research Design*. Thousand Oaks C.A: Sage Publications.

Fishman, J.A. (1991). *Reversing language shift: Theoretical and empirical foundations of assistance to threatened language*. Clevedon, England: Multilingual Matters

Foster, S.H. (1990). *The Communicative Competence of Young Children. A Modular Approach* London: Longman Publishers.

Furaha, J.H.(1991). *Matumizi ya lugha m jini Malindi: Jinsi mielekeo inavyoathiri uteuzi wa lugha*. Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Garry, T.H. (2009). *Practical Sampling katika Beckman L. na Rogled, J.D. The Sage and Book of Applied Social Research Methods*. SAGE Publication Inc.

Gaw, N. (2008). *We Have a Language Problem Here: Language Identity in East Africa* Swarthmore College Department of Linguistics.

Hebert Y. (1984). *The Socio-political Context of Native Indian Language Education in British Colombia*. The Canadian Journal of Native Studies.

Hudson R.A (1985). *Social Linguistics*. London: Cambridge University Press.

Hymes, D.H (1967). *The Anthropology of Communication in F.E. Dance Human*

Communication Theory. Original Essays New York.

Jeff, C. L. na Fasold, W.R. (1984). *An Introduction to Language and Linguistics*. Cambridge.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu Jamii*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taluma za Kiswahili.

Kioko, A.N. & Muthwii, M.J. (2001). 'Demands of a changing society: English in education in Kenya Today. In *Language, Culture and Curriculum* 8(7):128.

Kipacha, A. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kombo, D.K. & Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing*. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Kothari, R.C. (2004) *Research methodology: Methods and techniques*. New Dehli: New Age International (p) limited publishers.

Massamba, D., Kihore, Y. M na Msanjila, P. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I (1996). *Language policy in East Africa: A dependency Theory Perspective*. Nairobi: EAEP.

Msanjila, Y.P. (1999). *The Use of Kiswahili in Rural Areas and its Implications for the future of Ethnic Languages in Tanzania*. PhD Thesis, University of Dar es Salaam.

Muaka, L. (2009). *The dynamics of language use among rural and urban Kenyan youths*. University of Illinois. PhD dissertation

Mugenda, G.A. (2008). *Social Science Research. Theory and Principles*. Nairobi. Kijabe Printing Press.

Mulokozi, M.M. (2000). *Language, Literature and Forging of Pan-African Identity in Kiswahili*.
Vol 63.

Muthwii, M.J. (2002). *Language policy and practices in education in Kenya and Uganda: Perception of parents, pupils and teachers on the use of mother tongue, Kiswahili and English in primary schools*. Nairobi: Phoenix.

Mwita, M. (2001). *Language and Society: Kiswahili a National Language or a Special Class Language in Kenya. A Tool for Development. The Multidisciplinary Approach*. Eldoret: Moi University Press.

Okwany, L. (1993). *Attitudes of High School Students in Kenya Towards Learning of Kiswahili in Language of Instruction Policy Implication for Education in Africa 1997*. International Development Research Center. Canada.

Onyango, J.O. (1990). *Mielekeo ya Wasomi Kuhusi Matu,izi ya Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Richards, E. (1985). *Longman dictionary of applied linguistics*. Hong Kong: Longman Group Limited.

Rubanza, Y.I. (1979). *The Relationship Between Kiswahili and Other African Languages: The Case of Kihaya*. M.A Thesis, University of Dar es Salaam.

Su-Hie-Ting, (2003). 'Research on Language Planning on Language Attitude :Case Study in Sarawak'' Center for Language Studies,University Malaysia,Sarawak. *In Journal of Multilingual Development*, vol 24.

The Government of Kenya. (2010). *The Constitution*. Nairobi: Government Publishers

Thiba, M. (2000). 'We Speak Eleven Tongues: Reconstructing Multilingualism in South Africa.

In: Brock-Tune & R.K Hop son (eds) *Language of instruction for Africa emancipation: Focus on postcolonial context and construction*. Cape Town: CASS.

TUKI (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3) Nairobi: Oxford University.

Wamitila, K. (2008). *Kazi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers

Wardhaugh, R. (1986). *An Introduction to Social Linguistics*. Oxford: Basil Blackwell.



Mount Kenya University

KIAMBATISHO 1: FOMU YA IDHINI YA KUSHIRIKI KWENYE UTAFITI

Katika fomu hii, maneno “wewe, kwako na wako” yanayotumiwa yanamaanisha mshiriki wa utafiti. Maneno hayo pia yana maana ya mtu yeyote aliyeidhinishwa kutoa idhini inayohusiana na mshiriki katika utafiti huu lengwa.

Tafadhali unaombwa kushiriki kwenye utafiti utakaofanywa. Kabla ya kukubali kwako, lazima mtafiti akupe muhtasari wa taarifa muhimu ya kukusaidia kuelewa sababu zote zinazoweza kukufanya utake au usitake kujiunga na utafiti wenyewe.

Kabla ya kukubali kushiriki, hakikisha kuwa mpelelezi amekwambia yafuatayo:

- i) Sababu zote za utafiti, utaratibu utakaotumika kufanya utafiti pamoja na muda utakaoshiriki.
- ii) Hatari zinazoweza kutokea au usumbufu wowote unaoweza kuletwa kwako kutokana na utafiti utakaoshiriki.
- iii) Manufaa ya utafiti kwa jamii yote kwa jumla
- iv) Namna yote utakayosema au kufanya yatavyokuwa ya siri
- v) Warejelewa wote unaoweza kuwasiliana nao iwapo utakuwa na maswali, malalamishi au maoni kuhusu ushiriki wako.

Panapolazimu, ni sharti mpelelezi pia akwambie yafuatayo kwa uhakika:

- i) Fidia utakayopata iwapo mambo yatakuharibikia kinyume na matarajio.
- ii) Uwezekano wa hatari zozote zisizotarajiwa.
- iii) Mazingira yanayoweza kumlazimu mtafiti kukomesha kushiriki kwako.
- iv) Gharama za ziada unazoweza kukumbana nazo.
- v) Chochote kinachoweza kutokea iwapo utaacha ushiriki wako.
- vi) Wakati unaoweza kuambiwa mambo mapya yanayoweza kubadili mawazo yako kuhusu ushiriki wako.
- vii) Idadi yote ya watu watakaokuwepo wakati wa mchakato mzima wa utafiti.

Unaombwa kuelewa na kufahamu kuwa kushiriki kwako kwenye utafiti huu kutakuwa kwa hiari na iwapo utakataa kushiriki au labda kuachia ushirika katikati hutaadhibiwa wala kupoteza manufaa yoyote. Hatua yako kutia saina kwenye fomu hii kuna maana kuwa umeelezwa wazi kwa mdomo wa mpelelezi yote yanayohusu utafiti na kwamba umefanya maamuzi ya kushiriki. Ikiwa utakubali kushiriki, hakikisha umepewa nakala ya hati hii ikiwa imetiwa saina pamoja na muhtasari wa utafiti ulioandikwa kwa lugha ya Kiingereza kwa uelewa zaidi.

Iwapo unaweza kuwa na maswali, wasiwasi au malalamishi yoyote yale yanayolingana na utafiti huu basi una uhuru wa kuwasiliana na mpelelezi kwa kutumia nambari za simu kwenye muhtasari wa utafiti ulioandikwa. Iwapo utakuwa na wasiwasi kuhusu siri za haki zako za kimsingi ama labda unahisi kwamba unashuku mjadala wako na timu ya utafiti huu, usisite kuwasiliana na Wakili wa Ulizi wa Utafiti wa Binadamu kupitia nambari za simu zilizoandikwa kwenye muhtasari wa utafiti

uliondikwa na mtafiti.



Saini ya Mshiriki----- Tarehe...10/5/2024

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA SIASA: UMUHIMU WA MIELEKEO KATIKA KUTEUA LUGHA YA MJADALA BUNGENI KWENYE KAUNTI YA SIAYA

IDHINI YANGU YA KUSHIRIKI KWENYE UTAFITI

Mimi.....nakubali kushiriki kwa utafiti kwa hiari yangu. Naelewa kuwa hata nikifanya uamuzi wa kushiriki sasa, naweza kujitua au kukataa kujibu maswali yoyote bila ya hatua yoyote kuchukuliwa kwangu. Naelewa kuwa ninaweza kuondoa ithibati ya kutumia data yangu niliyoshirikisha kwenye mahojiano kwa muda wa wiki moja baada ya mahojiano. Hayo yakitokea data niliyotoa itafutwa. Nilipata nafasi ya kueleza kwa uwazi yote yanoyohusiana na utafiti na pia nikauliza maswali palipohitajia. Naelewa kushiriki kwangu kunahitaji kuwepo kwangu binafsi, muda wangu, siri zangu, kuongea kwangu kwa uwazi pamoja na kujibu maswali kwa ufafanuzi. Naelewa kuwa sitafaidika moja kwa moja na utafiti huu nitakaoshiriki. Nakubali kurekodiwa kwa mahojiano yangu na mtafiti au watafiti Ninaelewa kuwa ujumbe wowote nitakaotoa kwenye utafiti huu utachukuliwa kwa siri kubwa.

Ninaelewa kuwa kwa vyovyote vile kwenye matokeo ya utafiti huu, jina langu halitolewa wazi. Hili litafanyika kwa kubadili jina langu au kutaswiri ujumbe wangu vingine ili uwe siri kwa wapokezi au niliowasema wakati wa utafiti. Ninaelewa kuwa niliyosema wakati wa utafiti yanaweza kunukuliwa mbele ya bodi ya utafiti, kamati ya utahini ya chuo, kwenye miktadha ya uwasilishaji wa matokeo na kwa washikadau wowote waliotuma mpelelezi kufanya utafiti.

Ninaelewa kuwa iwapo nitamfahamisha wapelelezi kuwa maisha yangu au ya mtu mwingine yamo hatarini kuhusiana na utafiti nilioshiriki, wanaweza kuripoti kisa hiki kwa ofisi husika pakiwa na ruhusa yangu au hata bila ruhusa yangu. Ninaelewa kwamba fomu za idhini nilizotia saini yangu au rekodi za sauti zilirekodiwa wakati wa ushiriki wangu zitahifadhiwa kwa siri katika ofisi zote kwa muda fulani uliowekwa hadi pale bodi ya utahini itakapodhibitisha kazi zote za utafiti wa mwanafunzi.

Ninaelewa kuwa data zinazonihusu na ambazo zitafutwa kutoka kwa rekodi za utafiti zitawekwa siri kwa muda wa miaka miwili baada ya mwanafunzi kuwa na vikao na bodi za utahini. Naelewa kuwa chini za sharia za uhuru wa binadamu, ninaweza kufikia data nilizotoa wakati wa utafiti zikiwa kwenye ofisi zilikhifadhiwa. Naelewa kwamba nina uhuru wa kuwasiliana na yeyote aliyeshiriki kwenye upelelezi ili kusaka uwazi wa jumbe zote nilizotoa wakati wa ushiriki wangu.

JINA LA MTAFTI: **Oduor Atieno Winnie**
S.L.P. 14-40607,
Ukwala
Simu: 0707096386
Barua Pepe: atienowinnieoduor@gmail.com

WAREJELEWA

JINA LA MSIMAMIZI: **Dr. Alex Umbima Kevogo**
Chuo Kikuu cha Garissa
S.L.P. 1801-70100,
Garissa, Kenya.
Simu: 0724 961404
Barua Pepe: umbima2000@gmail.com

Chuo Kikuu cha Mount Kenya
S.L.P 342-01000,
Thika, Kenya.
254202878000
254709153000
Barua Pepe: info@mku.ac.ke

SAINI YA MSAILIWA



Saini ya Mshiriki.....

Tarehe.10/5/2024

Naamini kuwa mshiriki wa utafiti huu anapatiana idhini yake ya kushiriki katika utafiti



Saini ya Mtafiti.....

Tarehe.10/5/2024

KIAMBATISHO 2: RAMANI YA JIMBO LA SIAYA NA BUNGE LA KAUNTI

Siaya County and the Sub-Counties



COUNTY ASSEMBLY OF SIAYA



M

KIAMBATISHO 3: BARUA YA IDHINI YA KAMATI YA MAADILI (ERC)



Mount Kenya University

DIRECTORATE OF GRADUATE STUDIES

MAKI/2021/83692

11th June, 2024

*National Commission for Science Technology & Innovation (NACOSTI)
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P.O Box 30623- 00100
NAIROBI, KENYA*

Dear Sir/Madam,


RE: ODUOR ATIENO WINNIE - REGISTRATION NO. MAKI/2021/83692

The purpose of this letter is to introduce the above named student who is pursuing **Bachelor of Arts in Kiswahili** in the Department of **Psychology, Languages and Humanities** School of **Social Sciences**.

The title of the research is **"Matumizi ya Lugha Katika Siasa: Umuhimu wa Mifumo ya Katika Kuteua Lugha ya Mjadala Bungeni Kwenye Kaunti ya Siaya."** It has been cleared by the University's Ethics Review Committee (Certificate attached) and now has to proceed to the field to collect data between **June, 2024 and August, 2024**.

Any assistance accorded to the student will be highly appreciated.

Thank you.


Dr. Samuel M. Karenga, Ph.D
Director, Graduate Studies
Enc.

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 | +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified Institution.
Unlocking Infinite Possibilities

KIAMBATISHO 4: BARUA YA IDHINI(NACOSTI)



REPUBLIC OF KENYA



NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **932892**

Date of Issue: **04/July/2024**

RESEARCH LICENSE



This is to Certify that Ms.. **ODUOR ATIENO WINNIE** of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Siaya on the topic: **MATUMIZI YA LUGHA KATIKA SIASA: UMUHIMU WA MIELEKEO KATIKA KUTEUA LUGHA YA MJADALA BUNGENI KWENYE KAUNTI YA SIAYA** for the period ending : **04/July/2025**.

License No: **NACOSTI/P/24/37243**

932892

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code



NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

The National Commission for Science, Technology and Innovation, hereafter referred to as the Commission, was established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
 - i. Endanger national security
 - ii. Adversely affect the lives of Kenyans
 - iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
 - iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
 - v. Adversely affect the environment
 - vi. Adversely affect the rights of communities
 - vii. Endanger public safety and national cohesion
 - viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

KIAMBATISHO 5: HOJAJI YA WAJUMBE WA BUNGE LA KAUNTI

UTANGULIZI

Utafiti anaokusudia kufanya mtafiti, utalenga kufanya uchunguzi wa jinsi lugha inavyotumika wakati wa shughuli za bunge katika Kaunti ya Siaya. Kwa minajili ya kuhakikisha lengo hili limefanikiwa, unaombwa kujaza sehemu zilizo wazi katika hojaji hii. Katika masanduku yaliyoachwa wazi, kwenye sehemu ya A na ya B ya hojaji hii inatarajia utoe jibu lako kwa kutia alama ya (√) kulingana na jibu unalohisi liko sahihi ama utoe maelezo mafupi yanayohusiana na swali lililopo. Unahakikishiwa kuwa maadili yote yatazingatiwa kwa kuweka siri za jina la walioshirikishwa katika utafiti. Data itakayokusanywa kwenye utafiti huu itatumiwa kwa ajili ya utafiti huu peke yake wala haitatolewa mahali pengine popote kwa vyovote vile. Matokeo yatakayopatikana kwenye utafiti huu yatapendekezewa wajumbe wa majimbo nchini Kenya kuhusu dhima ya kutumia lugha iliyo na ufasaha inapolazimu kwa lengo la kufanikisha mawasiliano katika shughuli zinazohusiana na masuala ya siasa za serikali za magatuji.

SEHEMU A

1. Jinsia: Mwanamke Mwanamume
2. Una miaka mingapi
chini ya 25
Kati ya miaka 25 na 35
Kati ya miaka 35 na 45
Zaidi ya miaka 45
3. Umekaa katika Kaunti ya Siaya kwa muda upi?
Tangu kuzaliwa kwangu
Kati ya Miaka 10 – 15
Kati ya Miaka 5 – 10
Chini ya miaka mitano
4. Huwa unatumia lugha zipi?.....
5. Kwa sasa ni lugha ipi unayotumia kwa wingi?.....
6. Je, unazungumza lugha ipi kwa ufasaha zaidi?.....
7. Taja lugha nyingine yoyote unayoelewa na unayoweza kutumia kuwasiliana.
a).....
b).....
8. Je, wewe hutumia lugha gani unapongea na wananchi unaowawakilisha katika jimbo lako?
.....

9. Je, wewe hutumia lugha gani katika shughuli za kisiasa kuhudumia wananchi?

10. Je, wewe hutumia lugha gani katika mawasiliano ya mijadala bungeni?

11. Je, wewe hupendelea kutumia lugha ipi unapojumuika na wajumbe wenzio nje ya bunge?

12. Je, kunaweza kuwa na lugha zinazopendelewa kutumika katika mijadala ya bungeni katika kaunti yako?
 NDIYO LA

Iwapo jibu lako ni NDIYO, taja lugha hizo huku ukieleza namna zinavyotumika katika mijadala bungeni?

-
13. Taja lugha moja unayopenda kutumia wakati wa mjadala na wenzako bungeni?

14. Je, unaweza kuwa na sababu maalumu ya kupenda kuitumia lugha uliyotaja kwenye swali la (13) wakati wa mijadala bungeni? Unaombwa kutoa maelezo

15. Je, wewe ukiwa nje ya bunge hutumia lugha ipi?

16. Je, kunaweza kuwa na wakati wajumbe hutumia lugha zaidi ya moja katika mijadala bungeni?
 NDIYO LA
 Ikiwa jibu lako ni NDIYO, taja lugha hizo na utoe sababu za maamuzi hayo.

17. Je, wewe una marafiki wajumbe katika bunge wasiofahamu na kutumia Kiswahili katika mijadala?
 NDIYO LA
 Ikiwa NDIYO, huwa wanaotoa mchango kuhusu hoja iliyotolewa na mjumbe aliyetumia Kiswahili hutumia lugha gani kutoa mchango wao?

18. Je, ungepewa nafasi ya kupima umilisi wako wa Kiswahili ungesema aje?:
 Ni bora
 Ninakijua vizuri

Ninao ufahamu wa katikati

Sikijui kabisa

19. Je, ujuzi wako wa lugha ya Kiingereza ni wa kiwango gani?

Ni bora

Ninakijua vizuri

Nina ufahamu wa katikati

Sikijui kabisa

20. Miongoni mwa lugha zote unazozifahamu, ni gani unayopenda mno?

.....

.....

Kwa nini unaipenda mno kuliko lugha nyingine?

.....

.....

SEHEMU B

Katika masanduku yaliyoachwa wazi katika jedwali, onyesha tu msimamo wako kwa kuzingatia

kauli zilizoko kwa kutia alama ya (✓) .

| | Kauli | Nakubali kikamilifu | Nakubali | Sina Uhakika | Nakataa | Nakataa kikamilifu |
|----|---|----------------------------|-----------------|---------------------|----------------|---------------------------|
| 1 | Ni rahisi kujifunza Kiswahili | | | | | |
| 2 | Napendelea kutumia Kiswahili kutoa hoja zangu katika mijadala bungeni. | | | | | |
| 3 | Tunapotumia lugha ya Kiswahili,Wajumbe wenzangu huelewa ujumbe vyema zaidi. | | | | | |
| 4 | Lugha ya Kiswahili ina dhima kubwa kwa maendeleo ya taifa la Kenya | | | | | |
| 5 | Mimi hufurahishwa na kuchangamshwa na Vipindi vinavyotolewa katika lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari. | | | | | |
| 6 | Wanasiasa wengi katika kaunti yangu hupendelea kutumia lugha ya Kiingereza katika mijadala bungeni | | | | | |
| 7 | Licha ya kufanya mazoezi mengi, ninapata ugumu wa kuongea Kiswahili kwa ufasaha | | | | | |
| 8 | Kwa vile wanaonisikiliza hunicheka ninapokosea matamshi ya Kiswahili, Sipendi kukitumia. | | | | | |
| 9 | Ninapotaka wajumbe wenzangu wanielewe vyema wakati ninapotoa hoja zangu bungeni,mimi hupenda kuchanganya lugha. | | | | | |
| 10 | Mimi napenda kuwahutubia wananchi ninaowakilisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili | | | | | |
| 11 | Mimi huchagua Kiswahili kila mara ninapokabiliwa na uamuzi wa kuchangua kutumia lugha ya Kiingereza au Kiswahili. | | | | | |
| 12 | Mimi hujihisi shujaa kila ninapotumia lugha ya Kiswahili bungeni | | | | | |
| 13 | Mimi hupenda kutazama vipindi vya televisheni katika lugha ya Kiingereza | | | | | |
| 14 | Mimi nikiongea Kiswahili huwa sijihisi mtu mnyonge. | | | | | |
| 15 | Ningependa sana niwe na ujuzi wa kuwa na umilisi wa kuzungumza Kiswahili fasaha | | | | | |

| | | | | | | |
|----|---|--|--|--|--|--|
| 16 | Kiswahili huwa lugha yenye ufasaha kwa wingi | | | | | |
| 17 | Nachukia kusikiliza vipindi vya televisheni katika Kiswahili | | | | | |
| 18 | Matumizi ya Kiswahili yanapaswa kupigwa marufuku kwenye ofisi na mazingira ya kazini. | | | | | |
| 19 | Kiswahili ni lugha duni na isiyopaswa kulazimishwa itumike kitaifa | | | | | |
| 20 | Kiswahili ni chombo cha umoja kwa wakenya | | | | | |



KIAMBATISHO 6: MASWALI YA MAHOJIANO NA WAJUMBE WA BUNGE LA KAUNTI

Maswali ya kuongoza mahojiano na wajumbe wa kaunti.

1. Je, wakati wa mjadala bungeni, unapenda kutoa hoja zako ukitumia lugha ipi? Kwa nini unapenda kutumia lugha hiyo?.
2. Je, maoni yako ni yepi kuhusu kuchanganya lugha wakati wa mjadala ya bungeni? Unafikiri kuna uwezekano wa sababu zozote maalum zinazochangia kuwepo kwa hali hii?
3. Unapotangamana na wananchi unaowahudumia, unapenda kuwahutubia kwa kutumia lugha ipi? Unayo sababu yoyote?
4. Unafikiri lugha ya Kiswahili ina dhima gani kwenye mafanikio ya kisiasa katika kaunti yako na kwenye taifa la Kenya kwa jumla?
5. Je, wewe unapotaka kutoa hoja zako bungeni kuhusu mswada fulani hupendelea kutumia lugha gani? Kulingana nawe, utoaji hoja kwa Kiswahili unachangia kuelewa ujumbe huo kwa urahisi? Fafanua sababu za majibu yako.
6. Unadhani ni lugha ipi inayofanikisha mawasiliano kati ya wajumbe na wananchi mashinani katika shughuli za kimaendeleo?
7. Ni lugha unayoyazingatia kuwa ufasaha katika shughuli zote za bunge kwenye kaunti yako?
8. Je, wewe unadhani wananchi unaowakilisha wanapenda kuhutubiwa kwa kutumia lugha ipi? Je, kuna sababu yoyote inayowafanya wanamchi hao kuthamini lugha pendelewa?
9. Je, kuna dhima yoyote ya kufanya mjadala katika lugha za kikabila pamoja na Kiswahili katika bunge la jimbo lako? Fafanua sababu yako.
10. Je, Lugha ya Kiswahili ina dhima ipi kwako kama mjumbe na mwanasiasa kufanikisha kufaulu kwa harakati zako kikazi na kisiasa?



MATUMIZI YA LUGHA KATIKA
SIASA: UMUHIMU WA
MIELEKEO KATIKA KUCHAGUA
LUGHA YA MJADALA BUNGENI
KWENYE KAUNTI YA SIAYA

by ODUOR ATIENO WINNIE

Submission date: 13-Jun-2025 06:26PM (UTC+0300)

Submission ID: 2698428892

File name: Atieno_Winnie_Final_Draft_f.docx (1.56M)

Word count: 24512

Character count: 138090

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA SIASA: UMUHIMU WA MIELEKEO KATIKA KUCHAGUA LUGHA YA MJADALA BUNGENI KWENYE KAUNTI YA SIAYA

ORIGINALITY REPORT

| | | | |
|------------------|------------------|--------------|----------------|
| 13% | 11% | 3% | 6% |
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|-----------|---|---------------|
| 1 | Submitted to Mount Kenya University Student Paper | 2% |
| 2 | Submitted to Kenyatta University Student Paper | 1% |
| 3 | www.researchgate.net Internet Source | 1% |
| 4 | repository.out.ac.tz Internet Source | 1% |
| 5 | ir-library.ku.ac.ke Internet Source | 1% |
| 6 | Submitted to University Der Es Salaam Student Paper | 1% |
| 7 | pseudepigraphas.blogspot.com Internet Source | 1% |
| 8 | taifaleo.nation.co.ke Internet Source | <1% |
| 9 | repository.maseno.ac.ke Internet Source | <1% |
| 10 | www.coursehero.com Internet Source | <1% |
| 11 | ijojournals.com Internet Source | <1% |
| 12 | ir-library.mmarau.ac.ke:8080 Internet Source | <1% |

66 Melo, Silvia Maria Martins. "Emergencia e negociacao De Imagens Das linguas Em Encontros Interculturais Plurilingues Em Chat", Universidade de Aveiro (Portugal), 2021
Publication <1 %

67 elimumtandaoni254.blogspot.com
Internet Source <1 %

68 Basilio, Daniel Gomes da Silva. "Imagens reciprocas De Estudantes universitarios Portugueses e Turcos: Para Uma mediacao Intercultural Entre Portugal e Turquia", Universidade de Aveiro (Portugal), 2021
Publication <1 %

69 eprints.nottingham.ac.uk
Internet Source <1 %

Exclude quotes Off
Exclude bibliography Off

Exclude matches Off